
HABARI WANANDOA KORTINI MADAI YA KUMJERUHI JIRANI UK. 5

# Nipashe

Jumamosi Januari 20, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581561
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



**TAIFA STARS YATAKIWA KUIHESHIMU ZAMBIA**
UKURASA 24

**WABUNGE** CCM wasiowajibika kuwekwa kando
UKURASA 3



**WAGENI** zaidi wamiminika Dar kuingizwa kazini Mkuu wa KKKT
UKURASA 3

**CHADEMA** inavyoharibu mipango mizuri ya Rais Samia
UKURASA 8

# Magonjwa ya wazee yawatesa vijana



**YAMO** kisukari, shinikizo la damu, takwimu za WHO zashtua ... *Endelea ukurasa wa 2*



Ndege ya mizigo ya Shirika la (ATCL), 767-300F ikipakia mizigo katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta, jijini Nairobi, nchini Kenya juzi jioni na kuelekea nchini Dubai, baada ya zuio la ndege hiyo kutua nchini humo kuondolewa. Habari Uk. 5. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

UKURASA WA 16

## IVORY COAST BAADA YA MIAKA 40 AFCON ILE MATOKEO REDIONI SIKU YA PILI, SASA NI 'LAIVU'

"MPIRA. Timu ya taifa ya Cameroon imefanikiwa kutwaa Kombe la Mataifa Huru Barani Afrika kwa kuifunga timu ya taifa ya Nigeria mabao 3-1 katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny, Abidjan nchini Ivory Coast...

## Pinda asimulia maswali ya papo kwa papo yalivyompasua kichwa

UKURASA 4



## Kina Mdee wapiga hodi Mahakama ya Rufani

UKURASA 2

MICHEZO KRAMO 'OUT' SIMBA, YANGA MOTO ULE ULE UK. 24 KATUNI UK. 6




Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati), akifuatilia mkutano wa kimataifa wa mawaziri wa usafiri wa anga huko Hyderabad, India jana. Mkutano huo, unajadili fursa na changamoto za sekta hiyo. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga la Tanzania (TCAA), Hamza Johari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kina Mdee wabisha hodi mahakama ya Rufani

**Na Grace Gurisha**

WABUNGE 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiongozwa na Halima Mdee, wamewasilisha kusudio Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam la kukata rufani kupinga uamuzi wa mahakama hiyo kubariki uamuzi wa Kamati Kuu kuwavua uanachama.

Mbali na Mdee, wabunge hao ni Grace Tendega, Esther Matiko, Ester Bulaya, Agnesta Kaiza, Anatropia Theonest, Asya Mohamed, Cecilia Paresso, Conchesta Rwamlaza, Felister Njau, Hawa Mwaifunga, Jesca Kishoa, Kunti Majala, Naghenjwa Kaboyoka, Nusrat Hanje, Salome Makamba, Sophia Mwakagenda, Stella Fiyao na Tunza Malapo.

Kusudio hilo lililoandaliwa na Wakili wa wabunge hao, Ipilinga Panya na Edson Kilatu, liliwasilishwa jana mahakamani hapo na inakusudiwa kuwasilisha nakala ya taarifa hiyo kwa Bodi ya Wadhamini CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Mawakili hao wamewasilisha taarifa hiyo kwa ajili ya kujiandaa na hatua nyingine ya kwenda Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi uliotolewa na Jaji Cyprian Mkeha Desemba 12, 2023.

Wabunge hao wanakusudia kukata rufani dhidi ya sehemu ya uamuzi huo kama ilivyoamuliwa kwa baadhi ya sehemu ambazo hawajakubaliana nazo, hivyo hawakati rufani kwa uamuzi wote.

Katika uamuzi huo, Jaji Mkeha alisema mahakama haijafuta uamuzi wa Kamati Kuu wa kuwavua uanachama hao kwa sababu walipewa nafasi ya kujieleza lakini hawakutumia.

"Jamani shauri lililokuwa mbele yangu ni kwamba waleta maombi yaani Halima Mdee na mwenzake walileta maombi ya kuomba nafuu, waliomba mambo mawili kwamba Mahakama ifute uamuzi wa Kamati Kuu na uamuzi wa Baraza Kuu la Chadema, "alisema Jaji Mkeha

Jaji Mkeha alisema mambo mengi yaliwasilishwa na pande zote wakati shauri hilo linasikilizwa. Hoja hizo ziliweza kuzalisha mambo matano ambayo yeye aliweza kuyapatia majibu.

Alisema katika jambo la kwanza alijiuliza kwamba je, mjibu maombi wa kwanza (CHADEMA) kanuni zake zilikuwa zinaruhusu kusikiliza kwa dharula? Kwa sababu waleta maombi (Mdee na wenzake 18) walisema hawakupewa nafasi ya kusikilizwa.

"Na kama kanuni zinaruhusu, je, waleta maombi walipewa nafasi ya kusikilizwa? Na je, Kamati Kuu ilikuwa na hayo mamlaka ya kusikiliza mashauri kwa dharula? Majibu yangu hapa ni ndiyo kwamba kanuni zinaruhusu usikilizwaji wa dharula na pia waleta maombi walipewa nafasi ya kuieleza lakini hawakutumia," alisema Jaji Mkeha.

Pia alisema ukipewa wito ukaomba ahirisho sio lazima jibu liwe moja tu la upande wake, kwa sababu kuna kukubaliwa na kukataliwa, Mdee na wenzake waliomba ahirisho lakini lilikataliwa na kamati.

"Ikiwa kila mtu akipewa nafasi ya kusikilizwa, halafu hakutokea akaomba ahirisho limekataliwa, mwisho wa siku uamuzi utoke kwa upande wake unaweza ukaparalaizi mashauri yote yaliyokuwepo mahakamani," alisema

Alisema hoja ya tano, je, waleta maombi walisikilizwa na Baraza Kuu, jibu langu ni ndiyo kwa sababu waliwasilisha rufani zao kupinga uamuzi wa Kamati Kuu kuwavua uanachama. lakini shida ambayo ilikuwepo wanalalamika kwamba kuna baadhi ya wajumbe walikuwepo kwenye vikao vyote viwili.

"Hili halikubaliki sehemu yeyote ile, yaani watu waliokuwepo kwenye Kamati Kuu, wakae tena kwenye Baraza Kuu kutoa uamuzi hii haiko sawa kabisa,lakini kwa Sheria za Bunge ndiyo zinaweza kuruhusu hili, kwa hiyo nakataa maamuzi ya Baraza Kuu ambayo yalisikiliza rufaa hiyo," alisema

Mdee na wenzake 18, katika suala hilo walikuwa wanalalamika kwamba Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, walishiriki kikao cha Kamati Kuu na pia walishiriki kikao cha Baraza Kuu ambacho na chenyewe kilibariki woa kuvuliwa uanachama.

Kutokana na hali hiyo, Jaji Mkeha alitaka aeleweke kwamba hajafuta uamuzi wa Kamati Kuu kama walivyoomba waleta maombi kwa sababu walipewa nafasi ya kusikilizwa, lakini wao hawakutokea na pia hata katika viapo vyao wote walikiri kwamba walipokea taarifa kutoka kwa Katibu Mkuu, John Mnyika ya kuwataka wafike kwenye kikao hicho.

# Magonjwa ya wazee yawatesa vijana

**Na Pilly Kigome**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema magonjwa maarufu ya zamani kwa wazee sasa yanaongezeka na kuwatesa zaidi vijana.

Amesema hivi karibuni utafiti umeonyesha ongezeko la uwiano wa vijana wenye shinikizo la damu liliongezeka kutoka asilimia 0.2 hadi asilimia 25.1 Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Shirika la Afya Duniani (WHO), limeripoti ongezeko za aina tano za kisukari, aina ya kwanza miongoni mwa watoto na vijana kati ya mwaka 2011 na 2021.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana katika Mkutano wa Tano wa Kisayansi wa 'ARISE Network' wenye lengo la kubadili utafiti wa afya kwa vijana wa rika balehe na lishe kwa vitendo na sera zinazoweza kutekelezwa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema wakati maendeleo makubwa yamepatikana, dhahiri katika kupunguza matokeo duni ya lishe kama vile kudumaa kutoka asilimia 34.7 katika 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka 2018, anemia kati ya wanawake wa umri wa uzazi imepungua kutoka asilimia 44.8 2015 hadi asilimia 28.8 kwa mwaka 2018.

Vilevile, alisema kupungua kwa maambukizi mapya ya VVU ambapo baadhi ya maeneo ya vijana kama vile afya ya akili, bado yanahitaji juhudi zaidi.

"Tunahitaji ushahidi zaidi wa kisayansi ambao unaweza kuchangia kuimarisha utendaji wa sekta yetu ya afya na ushirikiano ulioonyeshwa hapa kwamba kuhusisha wanasayansi mbalimbali na wataalam wa afya ya umma wa ndani na nje ya Tanzania ambao ni mfano wa kuigwa.

"Nimefurahi kuona taasisi zetu za serikali kama Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Chuo Kikuu cha Dodoma, halmashauri mbalimbali za mikoa na wilaya, Taasisi ya Afya ya Ifakara, Taasisi ya MDH pamoja na ZAPHA+ kutoka Zanzibar zikiwa sehemu ya kazi hii," alisema.

Waziri Ummy amesisitiza umuhimu wa kuendeleza ajenda ya afya miongoni mwa vijana ili kuboresha afya na ustawi wao kwa ujumla. Pia alisema kuinua kizazi cha afya na watu wenye kinga kali, uwezo wa kufikiri kwa umakini na wenye ubora kitaaluma ambayo itachangia maendeleo ya taifa.

"Ninatoa wito kwa kila mmoja wetu, watunga sera, watafiti, watoa huduma za afya, wazazi, wanajamii na vijana kuibeba ajenda hii. "Mafanikio haya hayawezi kupatikana bila kushirikiana na washirika wa ndani na wa kimataifa na wafadhili," alisema.

Mtafiti Mkuu kwa upande wa Tanzania, Prof. Andrea Pembe, Daktari Bingwa wa Uzazi na magonjwa ya kina mama kutoka MUHAS, alisema utafiti huo umegundua wakiwapatia wajawazito dozi ndogo ya virutubisho vya madini ya chokaa (Calcium) milligram 500 sawa na kidonge kimoja kwa siku iliyopendekeza na WHO itasaidia kupunguza uwezekano wa kupata kifafa cha mimba kwa asilimia 50 na kuondoa kujifungua kabla ya wakati kwa asilimia 25.

Alisema utafiti huo ni wa kwanza na mkubwa kufanyika ambapo umehusisha wajawazito 11,000 kutoka Tanzania na 11,000 kutoka nchini India kuangalia ufanisi wa dozi hiyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Afya ya Jamii ya Africa(AAPH) Dk. Mary Mwanyika, alisema wamejikita katika utafiti wa afya ya jamii kwa kushirikiana na nchi tisa za Jangwa la Sahara.

Alibainisha kuwa utafiti huu ulifanyika ndani ya miaka mitano kwa kushirikiana na nchi za Afrika, Marekani na Ulaya.

Alisema utafiti zote mbili zilizofanyika kwa wanawake wa Tanzania na India umegundua madini chokaa ni muhimu yakianza kutumia, kwani yanaokoa maisha ya mama na mtoto.

HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel John Nchimbi (wa nne kulia) na viongozi wengine wakiomba dua kwenye kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Mjini Unguja, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamiminika kuingizwa kazini Mkuu wa KKKT

**Na Restuta James**

WAGENI kutoka ndani na nje ya nchi, wameendelea kuwasili kwa ajili ya ibada ya kumwingiza kazini Askofu Dk. Alex Malasusa kuwa Mkuu Mpya wa Kasnisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Ibada hiyo itakayofanyika katika Kanisa Kuu la Azania Front, itaongozwa na Mkuu wa Kanisa anayemaliza muda wake, Dk. Fredrick Shoo, ambaye pia ni Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini mkoani Kilimanjaro na mgeni rasmi atakuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, atakuwa mgeni rasmi katika ibada maalum ya kumwingiza kazini Mkuu mpya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kesho Jumapili itakayohudhuriwa na takribani watu 1,500.

Anayeingizwa kazini kuliongoza kanisa hilo kwa miaka minne ijayo ni Askofu Dk. Alex Malasusa, tendo litakaloongozwa na Mkuu wa sasa wa KKKT, Askofu Dk. Fredrick Shoo, anayeiongoza pia Dayosisi ya Kaskazini.

Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Goodluck Nkini, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa wageni wanaotarajiwa kuhudhuria tendo hilo ni 1,500.

Alisema ibada hiyo itaanza kwa maandamano yatakayofanywa na washarika walioandaliwa katika Kanisa Kuu la Azania Front.

"Tunategemea kuwa na viongozi wa kanisa kutoka sehemu mbalimbali duniani wakiongozwa na wawakilishi kutoka Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (WLF), maaskofu kutoka makanisa mbalimbali na vyama vya kidini. Pia tutakuwa na viongozi wa serikali watakaoambatana na Mheshimiwa Rais lakini pia kutoka vyama vya siasa vikiwamo vya upinzani," alisema.

Nkini alisema wamealika viongozi kutoka mihimili ya dola kama Bunge na Mahakama, viongozi wastaafu wa serikali na waandamizi kutoka taasisi za umma na binafsi nchini.

"Ibada itaanza saa 3:00 asubuhi itakayofuatiwa na tukio la kuingizwa askofu kazini ambayo yatafuatana. Baada ya hapo kutakuwa na sherehe fupi ya kumpongeza. Tunategemea eneo hili litakuwa na takribani watu 1,500," alisema Nkini.

Hata hivyo, alisema leo kutakuwa na ibada ya shukrani katika Usharika wa Mbezi Beach itakayoambatana na salamu kutoka kwa watu mbalimbali na baadaye chakula cha jioni.

"Ibada hiyo imepangwa ili kuifanya ile siku ya Jumapili (kesho), isielemewe...kwanza ni ibada ya Ushirika Mtakatifu, salamu na kwa wale watakaokuwa na zawadi wazitoe. Tutakuwa pia na chakula cha jioni ambacho tunatarajia watashiriki kati ya watu 1,000 hadi 1,200," alisema Nkini.

Nkini aliongeza kuwa watu wachache ndio watakaopata nafasi ya kutoa salamu za pongezi kwa Askofu Malasusa kesho.

Kwa mujibu wa Nkini, ibada hiyo itarushwa pia mubashara na vyombo kadhaa vya habari kikiwamo kinachomilikiwa na KKKT.

**ASKOFU MALASUSA**

Akizungumza na Upendo Media mapema wiki hii, Dk. Malasusa alisema watu wanahitaji uhuru wa kiroho na hasa kumjua Mungu.

Alisema katika utumishi wake, akiwa Usharika wa Yombo, Desemba 9, 2000 alifanikiwa kufungisha ndoa 54 kwa siku moja, tukio alilosema lilimwonesha namna watu wanavyohitaji uhuru wa kiroho.

"Uhuru wa kiroho ni kitu cha kuzingatiwa sana, ni uhuru ambao watu wengi sana wanauhitaji. Watu 108 na wasimamizi wao walifunga ndoa... baada ya kufunga ndoa zile niliona kulivyokuwa na mabadiliko makubwa kanisani," alisema.

# Wabunge wasiowajibika CCM kutoswa

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kuna timu maalum kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa wabunge, wawakilishi na madiwani na taarifa kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan.

Kimesema atakayeshindwa kuwajibika kwa wananchi hatapata nafasi katika uchaguzi ujao.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na wananchi wa Bunju ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara itakayofanyika katika mikoa 10.

Makonda alisema mwaka huu na mwakani, watawapima kwa namna gani wanatatua changamoto za wananchi na walivyo mstari wa mbele kukijenga chama.

Alisema alishaeleza tangu anakabidhiwa ofisi kuwa hatabeba mzigo, bali kila mtu ataubeba unaomstahili.

"Wabunge, wawakilishi na madiwani kama hamfanyi kazi ya utekelezaji wa Ilani na kama hamfanyi kazi ya kutatua changamoto za wananchi kwa sababu uhalali wa chama ni kutatua kero za wananchi. Hatuna haki kama hatutatui changamoto za wananchi. Ni jukumu letu kujitahidi kadri iwekanavyo kushughulikia matatizo ya wananchi," alisisitiza.

Makonda alisema kwa kauli moja watawapima kwa utendaji kazi na siyo kwa maneno au kugawa khanga kipindi cha uchaguzi kwa kuwarubuni wajumbe.

"Tutawapima si (kwa) kujipendekeza kwa viongozi bali kutaka kuwasikia wananchi wakieleza namna mbunge wao alivyowapigania katika kero.

"Tunataka kusikia wananchi wakisema mbunge fulani amewapigania kujengwa kwa shule au kituo cha afya, kauli hizo ni kigezo kimojawapo cha yeye kuchaguliwa tena na kuipeperusha bendera ya CCM," alisema.

Makonda alisema anayefanya kazi kubwa ni Mwenyekiti wa CCM kwa kuwa amekuwa akitafuta fedha, kujenga uhusiano na wao kazi yao ni kusema ili wananchi wapate kujua.

Alisema mikoa anayopita katika ziara kama mbunge hafanyi kazi na haonekani, kuna timu ya kutosha ya kuchukua taarifa na kuzipeleka kwa Mwenyekiti na kumweleza kuwa, 'tukienda na huyu tunapigwa.'

"Yapo mambo mengi yaliyofanywa na serikali ya CCM, lakini sauti zinazosikika ni chache na kazi ya mbunge kwa lugha nyepesi ni kupambania mgawanyo wa keki ya taifa," alisema.

Makonda alisema wakiona mbunge amechukua hatua ya ziada kutoa fedha za kwake maana yake hayo ni mapenzi yake zaidi kwa waliompigia kura.

"Lakini kazi kubwa ya mbunge kuliko zote ni kuhakikisha keki ya taifa wanapokaa Dodoma katika bajeti anapambania jimbo lake. "Kwa hiyo, wabunge wote wanatakiwa kufanya mikutano kabla ya kwenda bungeni kukaa na wananchi kujua changamoto zinazowakabili ili wakifika kule waongeze sauti," alisema Makonda.

Alisema wabunge hao wako ambao ni madiwani wanaingia kwenye mabaraza ya Halmashauri wakipambana kote hatua zinaonekana na wananchi wanaongeza upendo wao.

"Ninasema hivi tutahakikisha wanapatikana wabunge waadilifu, wachapa kazi, ili wawe sauti ya wananchi wanaowakilisha na mambo mazuri yaliyofanywa na Rais Samia yanatakiwa kuelezwa wananchi," alisema Makonda.

Akiwa eneo hilo, Makonda alipiga simu kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kumjulisha migogoro ya ardhi iliyoko eneo la Bunju nay eye kuahidi kwenda.

Makonda alisema ndani ya mwaka huu, serikali ina dhamira ya kufuta tatizo la umeme lililojengeka kama historia ya miaka mingi.

"Lakini chama kikahoji tulitaka majibu tukamuita Waziri wa Uchukuzi, Makame Mbarawa, na Masanja Kadogosa (Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Reli Tanzania) kwamba mbona kumekuwa na mabadiliko mabadiliko ya tarehe ya kuanza treni ya mwendokasi napo majibu yametoka na mwaka huu, kama kuna ahadi nyingine zaidi ya kuiona treni inatoka Dar es Salaam kwenda Dodoma wakatupa tena ahadi CCM itakula kichwa," alisema Makonda.

MAANDAMANO CHADEMA

Makonda alitaka Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu na Katibu Mkuu, John Mnyika, waulizwe kwa nini wanamkimbia kwenye mdahalo.

Alisema lengo la kuwaita ni kujenga uelewa wa pamoja na wananchi kujua kinachoendelea badala ya kukimbilia barabarani.

"Ninaomba niwakumbushe Watanzania walipokuwa wanakaa kwenye vikao hadi kwenye chama chao cha CHADEMA walihoji mbona mkienda kuongea hamtuambii mnaenda kuongea nini?

"Kwa wananchi hawajawahi kusema, leo wanasema ni maoni ya wananchi, hayo yalikuwa ni maoni ya kaka yangu Mbowe, Mnyika na Lissu, sio maoni ya wananchi," alisema Makonda.

Makonda alisema ili yawe ni maoni ya wananchi waende kwenye mdahalo na yupo tayari kukutana na viongozi hao ili wazungumze kwa pamoja, alafu wananchi wapime kama wapo tayari kwenda barabarani. Alihoji ni kwa nini wanataka kuwapeleka wananchi barabara kwa hoja zao binafsi na mikakati yao ya kutaka kuandamana hadi ofisi za Umoaja wa Taifa (UN) ni kutaka kuongeza maokoto.

"Mimi ninafahamu na hii taarifa nimeipata kutoka kwa mtu wa ndani kumbe kuna uchaguzi ndani ya CHADEMA Mnyika ameamua kumbeba Mbowe kwa vile anaona hawezi kumshinda Lissu.

"Na mule ndani wanalalamika Mbowe kumhujumu Lissu, kwa sababu hii agenda ya maandamano imeandaliwa ili imsaidie Mbowe aonekane kuna jambo kubwa la kitaifa analipambania alafu tarehe ziende mbele ili yeye aendelee kuongoza.

"Namuambia kaka yangu Mbowe aruhusu demokrasia ndani ya chama chake ukifika wakati wa uchaguzi ruhusu watu wachukue hiyo nafasi," alisema.

Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima, alisema changamoto kubwa ni miundombinu ya barabara na aliwahidi wananchi kuleta greda la matengenezo ya barabara na tayari ameshalinunua linasubiri kuanza kazi. Baada ya kauli hiyo, Makonda alimwahidi Gwajima kumpatia katapila 20 na kuanzia Jumanne zipite kwenye mitaa na kutatua changamoto za barabara zote za Jimbo la Kawe.

MAKALA

# Pinda asimulia maswali ya Papo kwa Papo yalivyompasua kichwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amesimulia milima na mabonde ya maisha yake, uteuzi katika nafasi hiyo na ugumu aliokutana nao ikiwamo maswali ya papo kwa papo bungeni, akiweka wazi kuwa yalimkosesha amani.

Pinda maarufu 'Mtoto wa Mkulima' anasimulia safari ya maisha yake kutoka Mwendesha Mashtaka hadi Waziri Mkuu, aliyehudumu kwa kipindi cha takribani miaka minane (2007-2015), wakati wa serikali ya utawala wa awamu ya nne, chini ya Rais Mstaafu Jakaya Kikwete.

Katika mahojiano maalum yaliyofanywa na Clouds FM, Pinda aliweka wazi kuwa katika miaka saba ya uwaziri mkuu, jambo lililomnyima usingizi ni maswali ya papo kwa papo, hivyo alitafuta njia ya kurahisisha suala hilo.

"Tulifanya jitihada kutaka kurahisishiwa si lazima swali hata eneo ambalo mbunge anataka kuuliza. Angalau tujue siku moja kabla ili kujiandaa kisaikolojia na kujiandaa vizuri.

"Yale maswali ni pale pale (papo kwa hapo) kila mbunge anakuja na jambo lake. Tulikuwa tunakaa na wasaidizi wangu ninasema, hebu jaribuni kubuni maswali na kuyajibu mniletee nisome lakini tuligonga mwamba.

"Sasa suala lile halikuwa jepesi, kuna wakati unapata shida kidogo kitu gani utaulizwa, unapata swali linauliza Zanzibar ni nchi au si nchi. Sasa ningekuwa nimeambiwa mapema, ningemwambia Rais hapo niweke namna gani. Sasa kinachobaki ni kutumia akili yako, ukiboronga huko huko tu tutajuana.

"Kidogo ilikuwa inakosesha amani ukisikia Alhamisi, (siku ya maswali ya papo kwa papo) aaah sijui pale (wabunge) watauliza nini? Uwezo binafsi ni msingi katika nafasi za uongozi na ndicho walichoona ni namna bora ya kuendesha papo kwa papo na ni kweli kama ungekuwa unajiandaa lisingekuwa jambo la kuvutia kama vile inavyokuwa," alisimulia.

Pinda alisema wakati mzuri ni ule ambao hakupata kitu chochote cha kumuudhi Rais.

"Wakati mzuri ni wakati wote ambao hupati kitu chochote unaona umemuudhi Rais wako, amekutuma jambo umefeli. Bahati nzuri tulikwenda vizuri na JK (Rais Mstaafu Jakaya Kikwete) na hajawahi kunifokea, uzuri wa nafasi hizi mnakuwa pamoja,"alisema.

**NAMNA ALIVYOPENDEKEZWA**

Kuhusu alivyopendekezwa kuwa Waziri Mkuu, alisema: "Bunge lilikuwa linaanza saa 11:00 jioni, nikaitwa kasoro dakika 20 na Rais. Wakati ule nilikuwa ninakaa Kilimani. Ilinishtua nikasema isije ikawa ndo hili hili maana yule kijana aliyenipigia aliniuliza wewe ndo Bwana Pinda? Uko wapi?

"Nikasema nipo nyumbani najiandaa kwenda bungeni, akajibu basi vizuri asante akakata, kumbe yuko njiani anakuja. Muda kidogo nikaona anaingia getini kijana mmoja hivi. Mimi nilikuwa ndani ninajaribu kuweka kasafari suti kakae vizuri, nikaambiwa kuna mgeni wako hapa nikasema ngoja nimalize kuvaa basi.



Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda.

"Akasema wanakuhitaji haraka kwa sababu ya majibu yale kidogo unaanza kuhisi kuna kitu kwa sababu nilikuwa Waziri wa Nchi labda mambo ya serikali za mitaa.

"Kwa hiyo nikatoka nikiwa na makobazi nikaenda, akasema ninaitwa na Rais sasa hivi, nikasema eeh! Nikasema ngoja nivae kidogo kwa nafasi yangu haikuwa ajabu kuitwa na Rais. Lakini tension (hofu) hiyo ya dakika za majeruhi ilikuwa kubwa kidogo. Akasema twende tu hivyo hivyo, nikamwambia ngoja nivae viatu, akasema 'twende hata na makobazi' nikasema ngoja nivae viatu, nikavaa akanipeleka kwa (Rais) Kikwete," alisema.

Pinda alisema alipofika Ikulu hakumkuta Rais Kikwete, akakaribishwa akakaa kusubiri na baada ya muda akaja.

"Akaja akasema kaka umekuja? Tukasalimiana tukakaa kwenye kochi ndiyo akatoboa siri, akasema nimekuita kwa sababu tuna hili pengo la Waziri Mkuu. Tumeona unaweza kutusaidia. Nilishtuka nikamwambia, lakini mzee kuna mawaziri wazoefu wengi tu, mimi nilikuwa Waziri wa Nchi juzi tu leo ndo Waziri wa TAMISEMI miaka miwili.

"Akanijibu akasema, haya mambo si uamuzi wa mtu mmoja ukiona hivyo tumeshirikishana ikaonekana gwanda hili ulivae wewe, nikamjibu basi Rais ninapokea ninajua upo utaniongoza vizuri.

"Tumetoka pale ananitia moyo lakini moyoni moyo unadundadunda kidogo nikawa ninajisemea Waziri Mkuu! Hii kitu mbona ngumu hii," alisimulia.

**KAMPENI ZA URAIS**

Pinda anafunguka kuwa mwaka 2005 wakati wa kampeni alifuatwa ili aingie katika kikundi cha Rais anayekuja, lakini alisita. "Nilifuatwa niingie kwenye kikundi cha Rais anayekuja nikasita ilikuwa mwaka 2005, nikaendelea na msimamo akaja mtu wa pili akasema tunahitaji mtu wa kutusaidia Rukwa huko.

"Nikasema hapana mimi kwa kuwa nimekuwa msaidizi kwenye ofisi hizi (Ofisi ya Rais) hiyo kazi nitaifanya, lakini kuja kwenye kujiunga huko Hapana. Sasa nilipopata hili la Uwaziri Mkuu, nikasema walinishauri niende huko nikasita.

"Nikasema kama hoja ndiyo basi amenisamehe tukamalizana vizuri, nikaenda Bunge mbio mbio nikapokelewa vizuri baada ya kutajwa jina, sasa nilipoambiwa kama una kahotuba kidogo nilipata shida hadi nilipostaafu nikawaambia wasaidizi wangu, hebu nendeni kwenye Hansard, angalieni siku ile nilisema nini? Nikatafutiwa nikaipitia nikasema kumbe nilijitahidi," alisimulia Pinda.

**NDOTO UWAZIRI MKUU**

Pinda alisema katika maisha yake hakuwahi kufikiria nafasi za juu kama Waziri Mkuu, kwa kuwa amesoma sheria alijua angepanda hadi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Alisema hata alipoitwa Ikulu kufanya kazi katika Ofisi Binafsi ya Rais (Mwalimu Julius Nyerere wakati huo), alishtuka na wakati huo alikuwa na umri wa miaka 30 na hakuwahi kujua watu wana siri kubwa.

UADILIFU

Pinda alisema mtu ambaye hana hofu ya Mungu hataona tabu kuiba serikalini na kwa mtu yeyote.

"Katika maisha ni wajibu watu tujikumbushe kuwa unapofanya hivi ni kosa mbele ya Mungu, unawaibia wananchi unastahili katika hali ya kawaida kwenda motoni. Pia malezi ya watoto kuna vitu vinatakiwa kujengwa kwenye malezi ukikaa na baba na mama akasema usifanye hivi ni vibaya kwa mwenzako," alisema.

Alisema sheria na taratibu za kiutumishi zinapaswa kuwa kali ili kuwa na watumishi na viongozi waadilifu.

"Siasa ni eneo jingine mtu anaona akifanya hivi ni sawa, uadilifu, uaminifu haijalishi upo kwenye siasa serikali au chama cha siasa lazima misingi iwepo kuwa na taifa ambalo tunajikuta tumejenga mila na desturi ambazo zinatupeleka kila mmoja kwenda.

"Sasa kama katika uchaguzi unatoa hongo unaona si tatizo, hili halipo sawa na mnataka ifike mahali kuliona ni jambo la kawaida si la kawaida,"alisisitiza.

**AKUNWA NA BBT**

Katika mahojiano hayo, Pinda alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuja na Programu ya Kilimo kwa Vijana (BBT) ili kuwahamisha kupenda kilimo na kuwa chanzo cha kuboresha maisha yao.

"Tuchukue hatua za kumfanya kijana apende kilimo na akienda kule aone kwamba alikuwa anaogopa bure, kirahisishwe aone ni jambo rafiki na aone tija. Mimi ni mtoto wa kwanza wa familia na baba alikuwa mkulima sikuwa na ujanja. Nimekuwa katika mazingira ya kushika jembe na ndoto ya kilimo haikupotea kila nilipokwenda," alisema.

Anasimulia kuwa alipomaliza chuo kikuu mwaka 1975, alipangiwa Mwanza akapata shamba eneo la Kisesa. Baada ya miaka miwili akatolewa na kupelekwa Mtwara kama Wakili wa Serikali Mwandamizi.

"Nilitafuta shamba (huko) ni kama kaugonjwa hivi. Baada ya mwaka mmoja nikaambiwa naitwa Ikulu. Niliacha shamba langu kama ilivyokuwa Mwanza. Nilipofika Dar es Salaam nilitafuta shamba liko Pugu milima ya Kisarawe ekari 20 lina miembe na miti mingine," alisema.

**SIRI KUONEKANA KIJANA**

Pinda anafunguka kuwa anafuga nyuki na ni mrinaji asali na ameanza kula akiwa mdogo na hiyo ndiyo sababu ya kumfanya aonekane kijana.

# Wanandoa kortini kwa madai ya kumjeruhi jirani

**Na Mwandishi Wetu**

KESI inayowakabili wakazi wa Dar es Salaam, Bharat Nathwani (57), maarufu kwa jina la Chiku na mke wake, Sangita Bharat Nathwani (54), inatarajiwa kuanza kusikilizwa ushahidi Februarri 19, mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Wanandoa hao wanashtakiwa kwa madai ya kumjeruhi jirani na kutoa lugha ya matusi.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya kiasia, wanaoishi mtaa wa Mrima, Kisuti kwenye jengo la Lohana, Dar es Salaam, walifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya, na kusomewa mashitaka yao na wakili wa serikali.

Katika hati ya mashitaka, washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa mashitaka manne, ambayo wanadaiwa kuyatenda Julai 21, 2023 ndani ya mkoa wa Dar es Salaam.

Katika shitaka la kwanza la kujeruhi linalomkabili Nathwani (Chiku) peke yake, anatuhumiwa kuwa Julai 21,2023 akiwa eneo la Mrima, Kisutu, jengo la Lohana ndani ya wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, alimjeruhi jirani yake.

Nathwani anadaiwa kumsababishia madhara makubwa mke wa jirani yake, Kiran Latit, kwa kuzamisha kichwa chake kwenye ndoo ya saruji na kumjeruhi katika macho na sikio na kwa kumpiga katika shingo, hivyo kumsababishia maumivu makali.

Katika shitaka la pili la shambulio la mwili linalomkabili Nathwani peke yake, inadaiwa tarehe hiyo na eneo hilo alimsababishia madhara jirani yake, Ratilal, katika mwili wake kwa kumpiga ngumi na mateke kichwani.

Shitaka la tatu na la nne yanayomkabili mke wake, Sangita, peke yake, anadaiwa kutoa matusi makubwa dhidi ya majirani zake, Lalit na Kiran kitendo ambacho kilisababisha fujo kwa namna ambayo inaweza kuzua uvunjifu wa amani.

Kesi hiyo ilitakiwa kuanza kusikilizwa Jumanne mbele ya Hakimu Lyamuya lakini ilishindikana kwa sababu hakimu huyo hakuwepo mahakamani kutokana na majukumu mengine aliyokuwa nayo.

Wakili wa Serikali, Frank Michael, alidai juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Franco Kiswaga wa mahakama hiyo kuwa kesi hiyo iliitwa kwa ajili ya kuanza kusikilizwa na pia wana mashahidi wawili na wako tayari kuendelea.

Mheshimiwa tunao mashahidi wawili na tupo tayari kuendelea, lakini tulikuwa tunaomba tarehe nyingine ya usikilizwaji kwa sababu hakimu anayesikiliza kesi hii hayupo," alidai Wakili Michael.

Hakimu Kiswaga aliwataka mashahidi hao kufika mahakamani hapo Februari 19, 2024 kwa ajili ya kutoa ushahidi wao.

" Mashahidi nawataka mfike tarehe hiyo na huyo shahidi ambaye amesema tarehe hiyo hatakuwepo atawasiliana na wakili wa serikali atatoa ushahidi wake kwa njia ya mtandao 'Video

# Ndege ya mizigo ATCL yatua Nairobi

**Na Joseph Mwendapole**

NDEGE ya mizigo ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)767-300F jana iliwasili katika Uwanja wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) jijini Nairobi, Kenya ambapo ilichukua mizigo na kusafirisha kwenda Dubai.

Hatua hiyo inakuja baada ya Tanzania na Kenya kuondoleana vikwazo vya biashara kwenye Sekta ya Usafiri wa Anga.

Alipoulizwa na gazeti hili jana kuhusu safari hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alikiri kuwa ndege ya mizigo ya ATCL iliwasili Nairobi ikitokea Dar es Salaam na kupakia mizigo yenye uzito wa tani 51. Mhandisi Matindi alisema ndege hiyo ilisafirisha shehena hiyo kwenda Dubai katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ambayo ni safari yake ya kwanza.

Alisema ndege hiyo iliondoka jijini Nairobi, usiku wa tarehe 18 Januari 2024 majira ya saa 3.30 na kuwasili Dubai saa 8:28 usiku na ilitarajiwa kurejea nchini jana.

Ndege ya mizigo iliwasili nchini Juni, mwaka jana ikiwa ya kwanza Afrika ya aina hiyona ilianza safari yake ya kwanza kwenda Dubai ikitokea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere (JNIA) Julai, mwaka jana, na imeendelea na safari hizo ikitokea nchi mbalimbali.

Safarizingine za ratiba ya ndege hiyo ni kati ya Dar es Salaam, Tanzania na Mumbai, India.

Aidha, nchi nyingine inazoendelea kuchukua na kupeleka mizigo ni Lusaka (Zambia), Nchi ya Afrika ya Kati, Harare (Zimbabwe) pamoja na Lubumbashi na Kinshasa (DRC).

Itakumbukwa mwanzoni mwa wiki hii Mamlaka ya Huduma za Anga Tanzania (TCAA) ilitoa tamko la kuzuia ndege za Kenya kutua katika viwanja vya Tanzania na baada ya mazungumzo baina ya nchi hizi mbili zuio liliondolewa jambo linaloongeza wigo wa kufanya biashara kwa nchi zote mbili.




Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Luteni Jenerali Salim Haji Othman (katikati) na Mkuu wa Tawi la Operesheni na Mafunzo, Meja Jenerali Ibrahim Mhona (kushoto), wakionyesha vitabu vya mafunzo ya ziada ya kuimarisha nidhamu na kuzuia unyanyasaji wa kingono na udhalilishaji wa kijinsia kwenye majukumu ya ulinzi wa amani, baada ya kuvizindua katika Kituo cha Mafunzo ya Ulinzi wa Amani Tanzania (TPTC), Kunduchi Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Kituo hicho, Brigedia Jenerali George Itang'sre. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# BoT yazindua mfumo sera ya fedha unaotumia riba

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imezindua mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba, huku ikitangaza riba kuu kati yake na benki nchini kuwa ni asilimia 5.5.

Akizindua mfumo huo mkoani Dar es Salaam jana, Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema hatua hiyo ni sehemu ya maboresho katika sekta ya fedha, yenye lengo la kuongeza ufanisi wa sera ya fedha.

Hata hivyo, Tutuba alitoa angalizo kwa wananchi akisema kuwa, kuanzishwa kwa mfumo huo mpya na kiwango hicho cha riba, haimaanishi kuweka ukomo kwa viwango vya riba zinazotozwa na benki na taasisi nyingine za fedha hapa nchini.

Tutuba alisema riba zinazotozwa na taasisi za fedha zitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko.

Alisema jukumu la BoT ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kudhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi. "Kwa takribani miaka 28 sasa, jukumu hili limekuwa likitekelezwa kwa kutumia mfumo wa ujazi wa fedha. Tulichagua kutumia mfumo huo kutokana na mazingira ya kiuchumi ya wakati huo," alisema.

Alisema mfumo huo ni rahisi kutumika kwa nchi zenye kiwango cha chini cha maendeleo ya masoko ya fedha na zenye changamoto ya upatikanaji wa takwimu za kutosha kwa ajili ya uchambuzi.

Tutuba alisema mabadiliko hayo yanafanyika ili kutekeleza itifaki ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika kuelekea kuwa na sarafu moja na Benki Kuu moja ya Afrika Mashariki.

Pia alisema yanafanyika kwa mujibu makubaliano ya jumuiya nyingine za kikanda ambazo Tanzania ni mwanachama. "Ni matumaini yangu kuwa riba hii ya asilimia 5.5 itatoa mwelekeo kwa taasisi za fedha katika utekelezaji wa shughuli zao, ikiwamo ukokotoaji wa riba za huduma zao na hivyo, kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kudhibiti mfumuko wa bei na kuimarisha shughuli za kiuchumi," alisema Tutuba.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Benki Nchini, Geoffrey Mchangila, aliipongeza BoT kwa kuanzisha mfumo huo pamoja na kuweka riba rafiki kwa benki.

Alisema malengo ya benki kuu yoyote duniani ni kudhibiti mfumuko wa bei, kwamba kwa kuanzishwa kwa mfumo huo kunakwenda kufanikisha adhma hiyo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dirisha dogo limefungwa rasmi, wachezaji jipangeni

**LIGI** Kuu Tanzania Bara ambayo hutoa mwakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inatarajiwa kuendelea tena baadaye mwezi huu.

Ligi hiyo yenye timu 16 kutoka mikoa mbalimbali nchini, ilisimama kwa ajili ya kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yaliyomalizika wiki iliyopita kwa Mlandege ya Zanzibar kutetea ubingwa ambao walikuwa wanaushikilia.

Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), zinazoendelea nchini Ivory Coast, Tanzania (Taifa Stars) ikishiriki michuano hiyo ni sababu nyingine muhimu ambayo ilipelekea ligi hiyo kusimama kwa muda.

Hata hivyo, Ligi Kuu Tanzania Bara ilisimama lakini dirisha dogo la usajili likifunguliwa na lilifungwa rasmi Januari 16, mwaka huu.

Msingi mkubwa wa usajili wa dirisha dogo ni kutoa nafasi kwa timu zenye mapungufu kujiimarisha kwa kusajili wachezaji ambao watakiongezea nguvu kikosi husika kwa ajili ya kufikia malengo kutokana na ushiriki wa mashindano mbalimbali.

Klabu pia hutumia dirisha dogo kurekebisha makosa ambayo iliyabaini katika mechi za mzunguko wa kwanza na ikitumia vyema nafasi hiyo, hupata matokeo chanya mara baada ya kurejea kwa ligi au mzunguko wa pili, kutokana na msimu husika.

Usajili huu unazihusu timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League pamoja na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo msimu mpya wa 2023/2024 ulianza rasmi Desemba 20, mwaka jana.

Mbali na usajili wa wachezaji wapya kutoka ndani na nje ya Tanzania, lakini zipo baadhi ya timu zilizoamua kuwatoa nyota wake kwa mkopo ili kwenda kuongeza uzoefu na wengine wakiomba kuondoka kwa ajili ya kuhitaji kupata changamoto mpya.

Hii yote imefanyika katika kipindi cha dirisha dogo, msingi mkubwa wa kila timu ni kurejea tena dimbani wakiwa wameimarika na tayari kukabiliana na ushindani watakaokutana nao.

Hakuna timu ambayo imefanya usajili katika dirisha dogo kwa misingi ya kujaza nafasi zilizokuwa wazi, tunaamini kila klabu imezingatia mapungufu waliyopokea kutoka kwa makocha wao na hatimaye kuongeza nguvu kwenye maeneo yaliyokuwa na changamoto.

Wakati dirisha dogo la usajili likifungwa, tunaamini kila timu imefanya kwa weledi zoezi hili kwa kutovunja mikataba ya wachezaji kinyume na taratibu na kujiepusha na adhabu ya kufungiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), kama ambavyo tumeshuhudia baadhi ya klabu zikikumbana na rungu hilo.

Mchakato huo umekamilika, kinachofuata ni wachezaji waliosajiliwa kujituma ili kuzipa matokeo chanya timu zilizowaamini na mwisho wa msimu kumaliza katika nafasi za juu huku wale waliokuwa kwenye hatari ya kushuka daraja, wakijinasua na janga hilo.

Mbali na kunusuru timu au kuisaidia klabu yako kufikia malengo, kila mchezaji anatakiwa afahamu kujituma na kucheza kwake kwa juhudi, kutaongeza thamani yake kuelekea msimu ujao, lakini pia kutamfanya ajihakikishe namba ya kudumu kwenye kikosi cha kwanza.

Wachezaji pia wanatakiwa wakumbuke Ligi Kuu Tanzania Bara ndio hutoa idadi kubwa ya wachezaji wanaounda kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), hivyo kama ndoto zao ni kuichezea timu, huu ni wakati wa kujifua na kujiweka tayari kuonyesha ubora mara baada ya ligi hiyo kurejea tena.

Kwa wachezaji ambao wamebaki Tanzania wakiwatazama wenzao wakipeperusha bendera ya nchi zao huko AFCON, wanatakiwa waanze kujipanga kukuza viwango vyao ili kuhakikisha nao wanakuwa sehemu ya nyota watakaocheza katika fainali zijazo.

Hakuna kisochewezekana, kila mchezaji ambaye amepata timu, anatakiwa ajipange kuhakikisha anaisaidia klabu yake kumaliza msimu wa 2023/2024 kwa kicheko huku wakiweka mbele nidhamu wakati wote wanapokuwa ndani na nje ya uwanja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Mashabiki Simba hawaeleweki wanahitaji nyota gani kikosini

**MIEZI** kadhaa nyuma, mashabiki wa Simba walikuwa wanalalamika kuhusu timu yao kutofunga mabao.

Kikosi chao kilionekana kina matatizo ya kutofunga mabao katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mashabiki hao hao walilalamika juu ya mastraika wao wakiongozwa na Mkongomani Jean Baleke, kukosa mabao ya wazi.

Ilianza msimu huu katika mechi za mwanzo za Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia. Mechi iliisha kwa sare ya mabao 2-2 huko Zambia, lakini Simba ilitawala karibuni kila kitu, na kama mastraika wake, hasa Baleke angetulia wangeondoka na ushindi usiopungua wa magoli matano.

Sare hiyo ilisababisha mechi ya Dar es Salaam kuwa ngumu. Na kweli ilikuwa ngumu kuliko ya kwanza kwa sababu Simba haikutawala tena mpira kama ilivyocheza mechi ya kwanza ugenini.

Ililazimika pia kusawazisha kama mechi ya kwanza ili kutinga hatua ya makundi. Ilitinga kwa msaada ya mabao mengi ya ugenini.

Uhaba wa mabao kwa mastraika wa Simba msimu huu umeonekana mpaka katika hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Imefunga mabao matatu tu katika mechi nne za Ligi ya Mabingwa Afrika ilizocheza kitu ambacho si kawaida kwa timu hiyo katika misimu yote iliyoshiriki michuano ya kimataifa kwenye hatua ya makundi.

Katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, timu inapata ushindi wa 'papatu papatu', ambapo timu inalazimika kufanya kazi ya ziada ili kupata ushindi.

Ushahidi mwingine ni kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi. Nako pia mastraika wa Simba wameshindwa kabisa kuonyesha cheche zao.

Mashabiki wakaendelea kupiga kelele wanahitajika mastraika ambao watakuja kutibu tatizo hilo.

Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, akaona isiwe tabu. Akaamua kuwatema, Baleke na Phiri ambao ndiyo mastraika vinara wa timu hiyo.

Badala yake amewasajili, Freddy Michael Kouablan, kutoka Green Eagles ya Zambia na Omar Jobe kutoka Zhenis ya Kazakhstan.

Mbali na hao, klabu ikawaacha Jimmyson Mwanuke, Shaaban Chilunda, Mohamed Mussa na Nassor Kapama, ikiwasajili Boubakar Sarr, Saleh Karabaka, na Ladack Chasambi.

Cha ajabu baada ya kusajili huo mpya kutangazwa, baadhi ya mashabiki wamegeuka tena na kuanza kupiga kelele kuwa kwa nini wamewaacha Phiri na Baleke?

Wanashindwa kukumbuka ni hao hao ndiyo walikuwa wanawapigia kelele kuwa siku hizi hawapo kwenye viwango vyao na hawafungi mabao.

Wengi wanapinga kuondolewa kwa sababu ya rekodi zao za nyuma kitu ambacho katika mpra hakipo.

Soka ni mchezo ambao mchezaji anaishi kwa rekodi za sasa, ndiyo maana hata Cristiano Ronaldo alipigwa panga Manchester United, aliporejea kwa mara ya pili kwa sababu hakuwa na kiwango bora kama yule CR7 wa kwanza.

Wamiliki, viongozi, benchi la ufundi na makocha hawakuangalia miaka ya nyuma aliwapatia mafanikio makubwa, walichoangalia ni nini anakifanya sasa?

Inaonekana mashabiki wa Simba hawajui nini wanakitaka. Wanataka mafanikio kwenye timu yao, au wanataka jina la mtu?

Benchikha ametaka aletewe mastraika wengine, watolewe waliokuwepo ili wasajiliwe wapya wenye makali zaidi yao baada ya kuwabaini kwa sasa hawawezi kuisaidia tena timu.

Hakuna mchezaji anayeweza kuendelea kukaa kwenye klabu yoyote kwa sababu ya hisani, eti kwa kubebwa na rekodi ya miaka iliyopita au msimu uliopita. Ndiyo maana kwa upande wa Yanga kwa sasa hayupo, Jesus Moloko, Djuma Shaaban wala Yannick Bangala na Simba hawana tena, Meddie Kagere, Chris Mugalu wala Mzambia Rally Bwalya.

Kama kuna mchezaji kipenzi kwa sababu ambaye hatosahaulika kirahisi ni Emmanuel Okwi, aliyewabeba Simba katika kila aina ya mashindano na kila aina ya mechi ngumu, lakini zama zake zilipopita aliondoka.

Ni hawa hawa viongozi waliowaleta kina Okwi, Kagere, Baleke, Phiri, ndiyo waliowaleta Kouablan na Jobe.

Ifike wakati mashabiki wa Simba waheshimu uamuzi wa makocha na viongozi wao waliowapa madaraka na sio kuponda au kulalamika kwa kila kitu ambacho wanakifanya.

Kwa sababu hata hawa ambao wameingia, wanaweza kufanya vizuri sana, lakini baadaye makali yao yatakapopungua wataondoka pia. Hiyo ndiyo asili ya mpira wa miguu.

Wanachama na mashabiki wa kweli siku zote wanachotaka timu yao ifanye vizuri tu, na siyo kwenye timu kuna mchezaji gani.

# Ardhi yapongezwa mabadiliko sheria udalali

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imeipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa marekebisho ya kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za mwaka 2023 katika Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

Akizungumza wakati wa wasilisho la taarifa ya marekebisho hayo jana jijini hapa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Ramadhani Suleiman Ramadhani, alisema wizara imezingatia mapendekezo ya kamati katika kufanya maboresho na kamati yake haina budi kuipongeza wizara kwa kazi nzuri.

"Wizara imezingatia mapendekezo ya kamati, hivyo niwapongeze kwa kazi nzuri ya kufanya marekebisho yaliyozingatia maoni ya Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo," alisema.

Mjumbe wa Kamati hiyo ambaye ni Mbunge wa Nanyumbu, Yahya Mhata, alisema maboresho yaliyofanyika yanonyesha wizara ilivyojipanga na kuipongeza hasa Katibu Mkuu ambaye ndiye mtendaji mkuu.

"Wizara iko 'smart' napenda niishukuru na kuipa pongezi kwa maboresho ya kanuni za madalali na zaidi nimpongeze mtendaji mkuu wa wizara," alisema Mhata.

Kaimu Mkurugenzi wa Sheria Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Method Msokele, aliwaeleza wajumbe wa kamati kuwa kanuni zilizofanyiwa marekebisho zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za mwaka 2023.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, aliishukuru kamati kwa ushauri wakati wa kufanya marekebisho ya kanuni za madalali na kuahidi wizara kusimama katika mhimili wakati wa kutekeleza majukumu yake.

"Niwashukuru sana wajumbe wa kamati hii. Mmetupa ushirikiano wakati wote wa maboresho ya kanuni za madalali na niwaahidi wizara yangu itasimama katika mhimili wakati wote wa kutekeleza majukumu yake" alisema.




John John (katikati), akipokea msaada wa meza na viti vyake 65 yenye thamani ya zaidi ya sh. milioni sita kutoka kwa Meneja Uhusiano kwa Jamii wa Mgodi wa kampuni ya Sotta Mining Ltd, John Bwana kwa ajili ya Shule ya Sekondari Nyantukuzanhwiga katika hafla fupi shuleni hapo, hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Husna Tony. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yawatahadharisha wazalishaji nondo na mabati

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wazalishaji wa mabati na nondo kuendelea kuzingatia ubora ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwa bidhaa hafifu.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Uandaaji Viwango TBS, David Ndibalema, wakati akizungumza kwenye mafunzo ya wadau wa uzalishaji wa nondo na mabati jijini Dar es Salaam.

Alisema nondo na mabati vinatumika kwenye shughuli za ujenzi hivyo ubora wake unapaswa kuzingatiwa kwa hali ya juu ili majengo yanayojengwa yawe salama na ya uhakika.

Alisema dhamira ya shirika hilo ni kujenga uchumi imara, endelevu na uliowa ushindani kwa kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na zinazoingizwa nchini zinakidhi matakwa ya viwango.

Ndibalema alisema ni jukumu la TBS kuendelea kutilia mkazo usimamizi wa viwango na kudhibiti ubora wa bidhaa ili kuhakikisha bidhaa zote zilizoko kwenye masoko nchini zinakidhi vigezo vya ubora muda wote.

Alisema lengo la mkutano huo maalum ni kukuza uelewa wa wadau wa uzalishaji wa mabati ili waweze kujua viwango vinavyokubalika kisheria na kuweka mikakati mahusus inayolenga kuweka viwango vya mabati.

Wataalamu wa TBS, alisema wamekuwa wakitoa elimu kuhusu matakwa ya viwango vya bidhaa za mabati na nondo vilivyowianishwa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupitishwa kwa ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Alisema wataalamu hao wamekuwa wakitoa elimu kuhusu taratibu za uingizaji nchini na ukaguzi wa shehena na mabati na nondo kutoka nje ya nchi ili kuendelea kukidhi viwango vinavyotakiwa.

"Hatua hii itawezesha kuwa na mwelekeo mzuri zaidi na wa kiweledi katika uzalishaji, uingizaji na usambazaji nchini wa bidhaa za mabati na nondo na TBS inatoa mafunzo haya ili mzingatie viwango kwa muda wote," alisema.

Aidha, alisema iwapo TBS itapata malalamiko kwa wanunuzi kuuziwa bidhaa zisizo na ubora haitasita kuwachukulia hatua wahusika ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Uzingatiaji wa Sheria wa TBS, Dk. Candida Shirima, alisema katika kutekeleza majukumu yake kisheria, shirika lina utaratibu wa kukutana na wadau kwa lengo la kuwakumbusha kuhusu matakwa ya sheria, kanuni na matakwa ya viwango.

Alisema lengo kubwa ni kuendelea kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zinazotoka nje ya nchi zinakidhi matakwa ya viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

"Na kwa bahati nzuri huwa TBS inawapa fursa nyinyi wadau wetu mnaohusika na uagizaji, utengenezaji na usambazaji mabati na nondo hapa nchini kutoa maoni yenu ili kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa na zile zinazozalishwa nchini zina viwango vinavyotakiwa," alisema .

# Mwananchi atoa ekari saba ujenzi wa shule

**Na Steven William,** MUHEZA

MKAZI wa Kata ya Mpapayu, Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Amina Waziri (65), ametoa mchango wake muhimu wa eneo la shamba lake ekari saba kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya serikali katika kata hiyo.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma, akizindua shule hiyo, alimshukuru mwananchi huyo kwa mchango huo, ambao sasa wanafunzi wameanza kusoma.

Mwinjuma alisema ujenzi wa awali wa shule hiyo ni ishara ya azma ya dhati ya kutoa mazingira bora ya kujifunzia wanafunzi ambapo mpaka sasa jumla ya Sh. milioni 105 zimetumika katika kujenga.

Alisema mpaka sasa shule hiyo ina madarasa manne na matundu manane ya vyoo na kuwapo kwake kumejibu changamoto ya watoto kutembea umbali wa jumla ya kilomita 14 kila siku kutafuta elimu ya sekondari katika kata nyingine.

"Katika kampeni za mwaka 2020, hii ni miongoni mwa kata zilizoniumiza kichwa kwa kuwa, ilikuwa na mazingira magumu zaidi kielimu.

"Kutokuwa na Shule ya Sekondari kata nzima kulifanya kwa miaka yote iliyopita wanafunzi watembee umbali mrefu kila siku na wengine waliacha shule, alisema.

Mwinjuma amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha na kusimamia maendeleo ya elimu na miradi mingine inayolenga kuinua hali ya maisha ya wananchi wa Muheza.

Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alitumia fursa hiyo kuwataka wazazi wote wilayani humo kuwapeleka watoto kuanza kidato cha kwanza

# CHADEMA inavyoharibu mawazo mazuri ya maendeleo ya Rais Samia

**Na Kambi Mbwana**

WAZIGUA wana msemo maarufu usemao 'Tindi dyahoswa nchereko' wakimaanisha kuwa siku zote mgomba unaponzwa na uzazi. Mgomba ukikomaa na kubeba mkungu wa ndizi, maisha yake yanakoma.

Mgomba unaokatwa baada ya kuzaa, huwa pembeni yake umechipua mwingine. Msemo wa kabila hili lenye asili Handeni mkoani Tanga, una maana kubwa. Umebeba ujumbe mpana. Hata kwenye ulingo wa kisiasa unajitokeza na kueleweka.

Unashabihiana pia hata kwa kuangalia mfumo na aina ya uongozi anaojaribu kuutumia katika madaraka yake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Mgomba kama mmea hauhisi maumivu hata pale unapokatwa. Si kwa binadamu kama Dk. Samia. Huumia anapoona dhamira njema aliyo nayo inashindwa kueleweka lakini kutokana na mamlaka makubwa aliyo nayo na anavyojitoa akiheshimu kila kundi ndani ya nchi, hakika alistahili uungwaji mkono kuliko ilivyo sasa.

Watu wanaojitokeza kulaumu, kushutumu na kukejeli huku wakiwa ni viongozi wa kisiasa kama ilivyo kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wanaendana na msemo kuhusu mgomba. Ingawa ni Rais wa nchi, lakini aina ya uongozi wake akiwa mama anayelea makundi yenye tabia tofauti, bado anaponzwa na uzazi wake.

Pengine asingekubali kuwa kiongozi, asingeghadhibika na karaha zinazofanywa kwa makusudi kutoka kwa watu ambao wengine amewasaidia kuendelea na siasa zao tofauti na ilivyokuwa katika uongozi wa awamu ya tano chini ya Hayati Dk. John Magufuli.

Wiki iliyopita, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alitangaza maandamano aliyoita ya amani.

Maandamano hayo alisema yatafanyika Januari 24, mwaka huu, kushinikiza serikali iondoe bungeni Miswada ya Sheria za Uchaguzi.

Kauli hiyo imekuja wakati Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ikikamilisha sheria iliyosomwa bungeni Novemba 23, 2023 mjini Dodoma.

Miswada hiyo ni Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023; Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 na wa Mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Kabla ya miswada hiyo kufikishwa bungeni kwa utaratibu wa kawaida, watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa walitoa maoni yao. Kwa sababu hii tu, CHADEMA wakiongozwa na mwenyekiti wao, wanaonyesha



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe

wanavyojaribu kutafuta njia ya kupandikiza chuki kwa jamii.

Mkutano Maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa uliofanyika Dar es Salaam Septemba 11 hadi 13, mwaka jana, na kushirikisha zaidi ya 500 wakiwemo viongozi mbalimbali wa kisiasa, uliokuwa na nia nzuri ya kujenga msingi wa haki na demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Mkutano huo haukuwa wa kwanza kwa kuwa awali ulifanyika jijini Dodoma kuanzia Desemba 15 hadi 17, 2021 na kuhudhuriwa na Rais Samia. Ni mkutano huo uliofanikisha kuundwa kwa kikosi kazi.

Pamoja na dhamira njema ya serikali, bado kuna watu wanaohamasisha maandamano wakisema ni ya amani! Hizi ni dalili kwamba CHADEMA wana kiu na shauku ya kurudisha nyuma nchi katika wakati huu ambayo kipaumbele ni uchumi kikishika hatamu.

Hakuna maandamano ya amani yasiyo na kibali. Kwa bahati mbaya, ili maandamano yapate kibali cha polisi, ni sharti wanahitaji pia sababu madhubuti ya kuandaliwa kwayo.

Kwa sasasababu haipo. CHADEMA wanasema wanashinikiza serikali iondoe miswada ya uchaguzi bungeni. Wanasahau ilipitia katika hatua zote zikiwamo za maoni ya Watanzania. Kama kweli itaondolewa bungeni, nuia njem,a ya Rais Samia ya kudumisha demokrasia na utawala bora itakuwa bure.

Ilishawahi kutokea kasumba kama hii wakati wa Awamu ya Nne, chini ya Rais Jakaya o Kikwete, uamuzi wa kusitisha mchakato wa Katiba Mpya ulifanywa baada ya chama hiki kususia hatua za mwisho.

Kulizuka mivutano kati ya serikali na CHADEMA. Kelele, malalamiko, shutuma na wakati mwingine kukejeliana hata kwa watu wenye heshima kukasababisha mchakato kuzimwa na serikali.

Shauku nyingine ya CHADEMA ni kutaka mchakato wa Katiba mpya uibuliwe. Bahati nzuri serikali ilishaweka hadharani hatua zitakazofanikisha ujio wa Katiba Mpya.

Kwa Tanzania inayoendesha siasa za vyama vingi, si jambo la manufaa kusikiliza mtazamo wa chama kimoja. Inafaa watu kukaa na kujadiliana pindi kunapoibuka mkivutano na hivyo ndivyo anavyopenda pia Rais Samia.

Kwa mtazamo wa CHADEMA, lengo lao ni kuivuruga amani ya nchi kwa faida zao binafsi. Wanafanya chokochoko ili serikali ivurugike wakiamini watanufaika. Kama hivi ndivyo wanavyowaza, ni wazi wanajidanganya. Ni vyema wakasukuma ajenda ya maeridhiano kwa njia ya vikao na wasijione wakubwa kuliko vyama vingine vya siasa.

Malengo yao, kwa bahato mabaya. hayawezi kufanikishwa kwa kuhatarisha usalama wa nchi . CHADEMA haina nguvu na upekee kuliko vyama vingine vya siasa. Kujiona wao wana uwezo wa kufanya lolote watakalo ni sahihi.

Vyama viheshimiane ili nao waheshimike mbele ya hadhira na hili likifanyika, nchi itaenda vizuri na kudumisha msamiati wa Tanzania kisiwa cha amani. Kuonyesha ubabe mbele ya mamlaka ni hatari kubwa na haya yamewahi kutokea miaka kadhaa iliyopita na kuathiri nguvu kazi ya taifa.

Ni kweli Katiba inaruhusu maandamano kama ilivyotajwa kwenye Ibara ya 20(1) lakini Sheria ya Polisi 43 (1) inataka watu watoe taarifa saa 48 kabla ya maandamano kuanza.

Katika sheria hiyo pia imewekwa wazi kuwa polisi wanaweza kuruhusu au kuzuia kufanyika kwa maandamano hayo kwa kuangalia hoja zao kama chombo cha ulinzi na usalama.

Wanaweza kusema wana uhaba wa polisi, majanga, ujio wa viongozi wajuu wa kitaifa nk. Na kwakuwa wao ndio wenye dhima ya ulinzi, itakuwa si jambo zuri kutokea mtu au kikundi cha watu kupinga hoja walizopewa na polisi.

Kama kikundi cha watu kitakaidi maelekezo halali ya wanaohusika na ulinzi wa watu na mali zao, si vibaya kama watatumia nguvu bila kuangalia madhara yanayoweza kutokea. Mwarobaini wa jambo hili ni watu kufuata sheria. Hakuna maandamano ya amani yasiyo na kibali cha polisi.

Hii ndiyo sababu madhubuti ya watu kuomba ulinzi pindi jamii inapohitaji maandamano. CHADEMA wanajua hili, ila wanalipuuza kwa sababu dhamira yao si kuandamana ili kushinikiza hoja zao zisikilizwe, ila kutafuta vurugu ili kuitusi serikali mbele ya marafiki zao wanaodhamini utendaji wa chama chao.

Huu ndio ukweli ambao Watanzania wote wanapaswa kuufahamu. Bahati mbaya wanafanya haya mbele ya Rais ambaye amekuwa rafiki na kipenzi cha demokrasia. Rais anayetaka watu wafanye siasa bila kuingiliwa. Rais anayetafuta namna nzuri ya kudumisha umoja, mshikamano, ushirikiano na maridhiano ya kisiasa.

**0712053949**



# Benki yaisaidia shule madawati

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

BENKI ya CRDB imetoa msaada wa madawati 50 kwa Shule ya Msingi Majengo iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida ili kuunga mkono jitihada za serikali kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Meneja wa CRDB Tawi la Manyoni, Hollo Gelleja, alisema kuwa benki hiyo imetoa msaada huo ili kuwawezesha wanafunzi kusoma vizuri na kutimiza malengo yao ya kupata elimu bora nchini.

Gelleja alisisitiza kuwa CRDB itaendelea kushirikiana na serikali kueleta maendeo kwa jamii ya wana Manyoni.

"Tunatambua Mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha wananchi wanapata huduma katika sekta ya elimu, afya na zingine na sisi CRDB tunasema mama hawezi kutembea peke yake lazima itembee na mama, itembee na Taifa, itembee na mwananchi, itembee na wanafunzi ndio maana tumekuja na 'Keti Jifunze' ambayo inamsaidia mwanafunzi kutimiza ndoto zake," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jimson Mhagama, alilishukru CRDB kwa msaada huo ambao alisema utawawezesha wanafunzi wa shule hiyo kusoma katika mazingira mazuri.

"Tunashukuru sana CRDB kwa msaada huu wa madawati naomba tuendelee kushirikiana na kutuunga mkono ili kuhakikisha jamii inapata huduma mbalimbali kama hizi," alisema.

Mhagama alisema bado wadau wa maendeleo wanahitajika kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kuwaletea wananchi maendeleo

Alisema mwaka jana serikali ilitoa fedha kwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya shule na bado itaendelea kusaidia sekta ya elimu katika halmashauri hiyo.

# Taharuki yatanda nyumba kuwekwa alama X

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa mitaa ya Amani na Ndachi Kata ya Nkuhungu jijini hapa, wamekumbwa na taharuki baada ya watu wasiojulikana kuvamia nyumba zao kuweka alama ya X.

Mmoja wa wakazi hao, Sharifa Ayoub, alisema juzi wakiwa kwenye nyumba zao, walivamiwa na watu hao na kuanza kuweka alama hizo na kuandika bomoa.

Sharifa alisema walipowahoji watu hao, walijibu kama wanataka kujua sababu ya nyumba zao kuwekwa X wafike chumba namba 42 cha ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupatiwa ufafanuzi.

"Walifika hapa na kuanza kuchora alama hizi nyumba zetu bila kushirikisha uongozi wa mtaa, hata gari walilokuwa wakitumia lilikuwa halina namba za usajili," alisema

Alisema waliwapigia simu viongozi wao wa mtaa ili kuwafahamisha kuhusu watu hao kuvamia nyumba zao na kuweka alama hizo kisha kutoweka.

"Tunaomba Waziri wa Ardhi. Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Jerry Silaa) atusaidie kwani kuna watu ambao wanadai kuwa wanahatimiliki ya maeneo haya ambazo zilishafutwa bado wanatusumbua," alisema na kuongeza:

"Tangu miaka mingi iliyopita tumekuwa tukiishi hapa kwa wasiwasi kwani kuna watu wanakamatwa na kupelekwa polisi, pia wengine wanapigwa na kutishwa." Abuu Kosta, alisema tangu mwaka 2013 wamekuwa wakinyanyaswa na watu hao wanaodai kuwa wamiliki halali wa eneo hilo.

"Tunanyanyasika sana, watu hawa wanatumia Polisi kututisha wakati tayari eneo hili tumepimiwa na kutambuliwa rasmi, lakini bado yupo mtu mmoja ambaye yeye ndiye anatusumbua lakini tayari wakati wa uongozi wa Waziri Lukuvi alimfutia hati yake na kusema asisumbue wananchi," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Amani, Aisha Kibwana, alisema wananchi wake wamekuwa wakipata usumbufu kutokana na watu hao wasiojulikana kuvamia eneo hilo na kudai wamiliki halali na kuwashinikiza kubomoa nyumba zao. "Hili suala limekuwa la muda mrefu iko siku watashindwa kuvumilia kutaibuka machafuko hapa, kabla ya kufikia huko tunaomba waziri mwenye dhamana aje," alisema.

Diwani wa Kata ya Nkuhungu, Daudi Mkandi, alisema wamefuatilia tukio hilo hadi ofisi ya halmashauri hiyo na kujibiwa haihusiki.

"Hiki kitendo ni cha kihuni kwani tumefuatilia katika ofisi zote kujua nani aliyehusika, hakuna aliyethibitisha kuhusika, hivyo wananchi wawe watulivu na sisi tutaendelea kulifanyia kazi," alisema Mkandi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (kulia), akizungumza na ujumbe wa Benki ya NMB, ulipomtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TANESCO: Wananchi anzisheni viwanda

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Dodoma limewataka wananchi kuanzisha viwanda kuzalisha bidhaa kutokana na kuwa na umeme wa kutosha katika kituo cha Zuzu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa TANESCO Dodoma, Donasiano Shamba kwenye kikao cha kuelelezea mikakati ya shirika hilo na miradi inayotekeleza kilichohudhuriwa na madiwani na polisi kata wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Shamba alisema ametoa rai hiyo kwa sababu Dodoma hauna uhaba wa umeme kutokana na uzalishaji mkubwa unaofanyika katika kituo cha Zuzu wa megawati 200.

"Mahitaji ya umeme ya Mkoa wa Dodoma ni megawati 61, hivyo kwa kiasi hiki idadi iliyopo sasa ya watumiaji Dodoma iwe mara mbili ndiyo itakidhi uzalishaji huu wa megawati 200, tunatoa wito kwa watu kuwekeza katika viwanda ili umeme huu utumike.

"Katika mwaka huu wa fedha (2023024) tumepatiwa kiasi cha Sh. bilioni 14 na kati ya hizo, bilioni 6 ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu yetu na kiasi kingine kupeleka umeme maeneo ya karibu na wananchi," alisema

Ofisa Usalama wa shirika hilo, Madega Dudu, alitaja changamoto wanazokabiliana nayo kuwa uharibifu wa miundombinu ya kusafirishia na kusambazia umeme, wizi wa vyuma, usalama, mafuta kwenye transifoma na nyaya za kopa.

"Tunaomba wananchi kutoa taarifa dhidi ya watu hawa ambao wanajihusisha na uharibifu wa miundombinu hii, tafiti zinaonyesha mafuta ya transfoma wanayoiba yanachanganywa na mafuta ya kukaangia chipsi kwa mikoa ya kanda ya ziwa na bahari wanakaangia samaki.

"Na wengine wanayatumia kwa ajili ya vipodozi na kiasi kikubwa yanatumika kutengenezea vilainishi vya mitambo," alisema Dudu





## Wananchi washauriwa kutoa ushirikiano kwa wadadisi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANANCHI wameshauriwa kutoa ushirikiano kwa wadadisi wa utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanyakazi nchini ili kuhakikisha takwimu zitakazopatikana zinaakisi malengo yanayokusudiwa.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Kazi, Idara ya Ajira, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji, Mustafa Hassan Makame kwenye zoezi la majaribio linalofanyika maeneo ya Michungwani Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Alisema utafiti huo ambao utafanyika baadaye mwezi huu, utaiwezesha serikali kufahamu uhalisia wa soko la ajira, nguvu kazi na ushiriki katika kupanga utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema pia utasaidia kujua idadi ya vijana wasiokuwa na ajira na wanaotakiwa kuajiriwa

"Dhamira hasa ya kutafuta viasharia hivi kuisaidia Serikali kupanga mipango ya kutatua changamoto ya ajira," alisema.

Ofisa Dawati la Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanyakazi Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Amina Mawazo Denge, alisema lengo ni kupata viashiria vya taarifa za soko la ajira na kuiwezesha serikali na wadau wa maendeleo kupanga na kuhuisha mikakati ya ajira nchini.

"Utafiti huu una viashiria vingi muhimu vinavyohusiana na mambo ya ajira nchini. Ni vyema wananchi kushirikiana na watafiti kufanikisha malengo ya serikali," alisema na kuongeza kuwa:

"Utafiti huu utaisaidia Zanzibar na Tanzania kukakikisha inaandaa mikakati ambayo itasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana."

Sheha wa Michungwani, Fauzia Omar Mahawi, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa wadadisi kwa vile taarifa zao zitakuwa siri na kwa ajili ya matumizi yaliokusudiwa na serikali.

Baadhi ya wananchi walioohojiwa kwenye utafiti huo, walisema watahakikisha wanatoa taarifa sahihi zitakazoiwezesha serikali kuzitafutia ufumbuzi changamoto za ajira hasa kwa vijana na wanawake.

Zoezi la utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanyazi linatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu nchini.

Kwa mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2021 na kwamba litakuwa likifanyika kila mwaka badala ya miaka mitano.

# Dk. Nchimbi atema cheche Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi amesisitiza CCM itahakikisha inasimamia maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa kwa kuwa ndio njia pekee ya kuimarisha na kudumisha amani visiwani hapa.

Dk. Nchimbi aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza na wafuasi wa CCM katika Ofisi Kuu za chama hicho zilizopo Kisiwandui baada ya mapokezi makubwa yaliyoambatana na matembezi yaliyoanzia Michenzani.

"Nataka niwahakikishieni CCM chini ya mwenyekiti wake, Dk Samia (Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan) itaimarisha usimamizi wa serikali zake (Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ)) , kuhakikisha inatimiza wajibu kwa kutekeleza ilani na kuwatumikia wananchi kwa uadilifu mkubwa," alisema.

**SERIKALI YA UMOJA WA KITAIFA**

Alisema chama hicho kina msimamo usioyumba kuhusu umoja, utulivu na mshikamano wa nchi na ndiyo sababu kitaendelea kuunga mkono uwepo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Nchimbi alisema waliozaliwa juzi wanaweza wasifahamu maana ya siasa za kiuhasama zilizokuwepo Zanzibar, ambapo watu wa familia mmoja walihasimiana, lakini kuna wanaoona kama SUK haina umuhimu wakati imesaidia kuwepo kwa utulivu na amani nchini.

Alisema mtu ambaye anaona serikali hiyo haina umuhimu, hajali maisha ya Watanzania na Wazanzibari na mwenye hamu ya kuona ikivunjika, wanatamani kunusa damu za watu, hivyo lazima wana CCM kushirikiana na kutoyumba na kuiunga mkono.

**SHIME ACT WAZALENDO**

"Tunawapa shime wenzetu wa ACT Wazalendo wajue nao wanawajibu wa kuunga mkono Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kama kuna mambo madogo madogo tuzungumze ndio maana ya maendeleo na mashirikiano, lazima tujue wote ni Watanzania na suala la kupendana ni wajibu wa kiraia," alisema.

Alisema CCM ipo tayari kuendelea kushirikiana na ACT Wazalendo kwani ni sehemu ya kuenzi Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu waasisi wake hawakukusudia kuwa na nchi iliyojaa uhasama, chuki na isiyo na umoja.

"Haya hayakuwa matarajio ya waasisi wa nchi yetu, waasisi wa chama chetu, waasisi wa Mapinduzi lazima wote tushirikiane tuziunge mkono serikali zetu kwakila inavyowezekana," alisema na kuongeza:

"Nimekutana na makamu wetu wa CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi (Rais wa Zanzibar) nimemuuliza unafikiri nini kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa akaniambia ni muhimu sana kwa Zanzibar na Tanzania nikasema Alhamdulillah."

Katibu mkuu huyo, alisisitiza kuungana na kuwa kitu kimoja na kuwataka wana CCM kuvunja makundi.

" Unapotaka kupika unawasha moto lakini unapopakua unazima moto wako, ni mjinga peke yake anayekoleza moto wakati ameshapakua, utakufa kwa joto," alisema.

**WALIOSHINDWA, KUSHINDA**

Alisema wale walioshinda katika chaguzi wanatakiwa kuwa wanyenyevu na walioshindwa lazima wajue kushinda na kushindwa kupo kwenye mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Alitoa mfano kuwa amegombea mara 27 na kushindwa mara sita na wala haikuwa shida kwake.

Alisisitiza kuwa ukiamua kuwa mwanasiasa lazima ukubali kushindwa. "Mimi ni muumini wa mambo ya Zanzibar hata leo (jana) asubuhi wasaidizi wangu wameona niseme katika chai ya asubuhi sitaki chochote nataka nile urojo na ninamapenzi makubwa na Zanzibar na nina madeni makubwa ya malezi ya viongozi kutoka Zanzibar na katika kuandaliwa kwake kuwa kiongozi Zanzibar ina mchango wa kipekee " alisema.

**WANACCM WAMPONGEZA**

Wakizungumza baada ya mapokezi hayo, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM, sasa ni mjumbe wa wadhamini wa chama hicho, Vuai Ali Vuai, alimpongeza Dk Samia kwa kupendekeza jina la Dk. Nchimbi kwa kusema ni chaguo sahihi hasa kwa wakati wa sasa.

"Nasema haya kwa sababu ni mtu ninayemfahamu mwaka 1998 ndiye aliyeanza kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Vijana wa CCM Tanzania na wakati huo huo na mimi nikachaguliwa kuwa katibu mkuu wa umoja wa vijana CCM Tanzania, " alisema.

Vuai, alisema Dk Nchimbi ni mtu anayemfahamu kuwa ana uwezo mkubwa wa uongozi, anaifahamu CCM na jumuiya zake.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa katika mazungumzo na Uongozi wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), ukiongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Dk. Isaack Shimba (wa pili kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu, Adam Mihayo katika Ikulu Zanzibar hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wilaya ya Mjini kinara udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya udhalilishaji wa kijinsia visiwani hapa kuripotiwa kupungua kwa kwa kipindi cha mwezi mmoja mwaka jana hadi kufikia 162, Wilaya ya Mjini imetajwa kuongoza kwa matukio hayo.

Kwa mujibu wa Meneja wa Divisheni ya Jinsia na Ajira kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Sabina Raphael Daima, takwimu hizo ni za matukio hayo yaliyopungua kwa mwezi huo wa Disemba kutoka 172 yaliyoripotiwa kutokea Novemba mwaka jana.

Sabina, alisema katika matukio hayo 162, waathirika wengi ni watoto kwa asilimia 81.5, wanawake (14.2) na wanaume (4.3).

Alisema miongoni mwao wasichana 101 sawa na asilimia 76.5 na wavulana 31 sawa na asilimia 23.5.

Alisema matukio ya kubaka na kuingilia kinyume na maumbile yameripotiwa kupungua kwa mwezi huo wa Disemba mwaka jana.

Alisema kulingana na takwimu hizo, idadi ya matukio hayo kwa mwaka imeongezeka kwa asilimia 5.2 kutoka 154 yaliyoripotiwa Disemba 2022, hadi kufikia matukio 162 ya Disemba 2023.

Sabina alizitaja wilaya inayoongoza kwa matukio ya ukatili na udhalilishaji kuwa ni ya Mjini ikilinganishwa na wilaya nyingine kwa kuwa na matukio 41 sawa na asilimia 25.3.

"Inayofuata ni Wilaya ya Magharibi A Unguja yameripotiwa matukio 33 sawa na asilimia 20.4. Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio manne sawa na asilimia 2.5 ikilinganishwa na wilaya nyingine," alisema.

Kwa upande wa ubakaji, alisema Mjini inaoongoza kuwa na idadi kubwa ya matukio 13 sawa ma asilimia 18.3 ya vitendo hivyo, ikilinganishwa na wilaya nyingine.

"Kati ya matukio 72 ya ubakaji yaliyoripotiwa kwa mwezi wa Disemba 2023, matukio 11 ya ubakaji sawa na asilimia 15.3 yameripotiwa kwa wanawake na 61 kwa wasichana sawa na asilimia 84.7," alisema

Alisema kati ya matukio hayo ya Desemba, 132 sawa na asilimia 81.5 yanafanyiwa uchunguzi na polisi, 28 sawa na asilimia 17.3 yapo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mawili saw ana asilimia 1.2 majalada yake yamefungwa na Polisi.

Sabina alisema kwa mwaka jana kulikuwa na matukio 1,954 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yaliyoripotiwa na waathirika 1,959.



**ROMA**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JANUARI 20, 2024



# HANA KOROMEO?

Kuna usemi kwamba wanaume wameumbwa na koromeo kooni ili kumwezesha kuwa na uvumilivu na kuhifadhi mambo mengi yanayoumiza.

Hata hivyo, katika sakata la Baba Levo na mke wake Salma Mdoli maarufu kama Mama Ruby, watu mbalimbali wamejitokeza kutoa maoni yao na wengi wanamlaumu Baba Levo kwa kudai hana sifa hizo na kuwa chanzo cha kuendeleza mgogoro huo.

Baadhi ya watu wamedai kwamba Baba Levo ameonekana hana uvumilivu na subira, badala yake amezidi kuuwasha moto kutokana na kauli zake tata alizozitoa kupitia vyombo vya habari.

Chanzo cha ugomvi huo ni baada ya mama Ruby kumlalamikia msanii wa vichekesho Asmah kwamba anataka kuvunja ndoa yake na kumtahadharisha amuache mume wake.

Moto ulilipuka zaidi baada ya Baba Levo kurejea kutoka safari yake ya kikazi nchini China akiwa na zawadi kwa ajili ya Mama Ruby na Asmah. Jambo hilo lilimkera Mama Ruby, na aliamua kumkemea.

Kwa upande wake, Baba Levo akizungumza kupitia kituo kimoja cha redio, amemlaumu mama Ruby kwa kutokuwa na heshima na kwamba hawezi kumuacha Asmah kwa matakwa yake kutokana na mema aliyomfanyia wakati alipopitia mengi yaliyofanywa na mke wake.

Baadhi ya watu wakiwamo wasanii maarufu, wameingilia kati suala hilo na kuwataka wote wawili wajizuie kutoa maneno makali hadharani wakitambua wao ni wanandoa wanaweza kuyamaliza kwa mazungumzo.

Mtangazaji na msanii wa filamu, Mwijaku amemlaumu Baba Levo kwa kuendeleza malumbano hayo kupitia kituo cha redio kwani haitatui tatizo hilo kama anavyofikiria.

"Huwezi kumsema mke wako kupitia redioni, huko ni kukosa nidhamu na maadili. Lazima tutambue ugomvi wa ndani huishia ndani huko huko na kuleta nje ni vibaya na haipendezi," amesema Mwijaku.

Ameshauri baba Levo, kurudi nyumbani kwake na kuzungumza na mama Ruby katika hali ya utulivu na kupata suluhu itakayodumisha mapenzi yao.

BASI SAWA

## Roma awaingiza watu kwenye kifo




WATU wengi wamefuata nyayo za msanii wa rap nchini, Roma Mkatoliki, kwa kutembelea mtandao unaotabiri siku ya kifo chao.

Hivi karibuni Roma Mkatoliki aliwashangaza mashabiki zake baada ya kudai kwamba ametabiriwa kifo chake kitatokea mwaka 2028.

Kupitia ukurasa wake wa X, Roma alichapisha kwamba mtandao wa Google umetabiri kifo chake kitatokea Januari 12 mwaka 2028 ndio itakuwa mwisho wa uhai wake.

Baadhi ya mashabiki waliufuata mtandao huo na kutafuta neno 'Death Clock' na kisha walimjibu na wao pia wamepatiwa siku zao za mwisho za kuishi duniani kama ilivyo kwa msanii huyo.

## Leah Fashion awatisha mastaa wa mitindo



MREMBO anayekuja kwa kasi kwenye tasnia ya burudani na mitindo Bongo, Leah Fashion, ametamba kuwa mwaka 2024 atawatesa mastaa kwenye majukwaa mbalimbali ya mavazi.

Akizungumza na BT, Leah amesema tayari ameweka mipango yake sawa, hivyo mashabiki wa mitindo na ubunifu watarajie kumuona kwenye majukwaa makubwa akinadi mavazi.

"Hao mastaa kwenye tasnia wajipange, kazi yangu inaongea nadhani mwaka huu nitawakimbiza wakongwe kwa kazi za kibunifu kwenye majukwaa na hata mitandaoni," amesema Leah Fashion ambaye anapatikana kupitia Instagram @Leahfashion



# DIAMOND HABANDUKI PENZI LA ZENJI

HATIMAYE bosi wa lebo ya muziki ya WCB, Naseeb Abdul, maarufu kama Diamond Platnumz ameonekana kubadilisha mtazamo kwa kusisitiza ataendelea na uhusiano wa kimapenzi na Zuchu.

Hivi karibuni baada ya mama yake kusisitiza kwamba hatambui mapenzi ya mtoto wake na Zuchu Diamond aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kwamba yuko singo.

Hata hivyo baada ya siku mbili, alibadilisha msimamo huo na kueleza kwamba hawezi maisha ya upweke na badala yake ameamua kuendelea na mpenzi wake kutoka Zanzibar yaani Zuchu.





# Sallam SK yote amtupia Mungu

TUKIO la kuungua moto studio ya redio ya Mjini FM, mmliki wake ambaye pia ni meneja wa Diamond Platnumz, Sallam SK amewashukuru Watanzania kwa kuwa naye bega kwa bega katika tukio hilo.

SK kupitia ukurasa wake wa Instagram aliweka picha za studio hiyo iliyoungua moto na kueleza kila kitu kinapangwa na Mungu, hata hivyo aliumia sana.

Amesema kwamba kituo hicho cha redio kimesharejea hewani na kazi zinaendelea kama kawaida.

FILAMU

## Msuto Daily: Umbea utakukondesha

Na Adam Fungawango

KWA wale wanaoishi kwenye nyumba za kupanga mjini, au hata kujenga nyumba uswahilini wanajua jinsi gani huko watu wanaishi.

Wenyewe wanakuita 'uswazi.' Ni sehemu ambayo wanaishi watu mchanganyiko, kutoka kwenye mikoa tofauti, utamaduni tofauti, mazingira tofauti na hata malezi tofauti.

Sasa wanapokutana pamoja, hasa kwenye nyumba za kupanga inakuwa balaa.

Filamu ya 'Msuto Daily', imelenga si tu kuburudisha, lakini pia kufundisha na kuelemisha, kukanya juu ya tabia ya kufitinisha watu.

Imchezwa na Riyama Ally, Ally Salum Mboto, Selemani Barafu, Diana Kimaro, Ummy Mohamed, Maina Thadei, Najma Ally, Zainabu Ally na wengineo.

Riyama ambaye anacheza kama 'Mama Tatu' ni mke wa Mboto. Wanaishi nyumba ya kupanga.

Lakini tabia ya Mama Tabu ni kugombanisha wapangaji wenzake.

Akawagombanisha mtu na dada yake wa baba mmoja, lakini mama tofauti ambao walikuwa wakiishi chumba kimoja, lakini akatumia lugha ya ulaghai kila mmoja akimpa maneno ya uongo na akafanikiwa kuwagombanisha.

Akamgombanisha mpangaji mmoja na mkewe, kiasi kwamba nyuma ikawa hailiki wala hailaliki.

Kuna mtu na rafiki yake mabachela ambao walikuwa wanaishi chumba kimoja, nao akawaingilia na kuwagombanisha kwa maneno ya uongo, akaenda kwa yule asiyelipa kodi na kumwambia mwenzake anamsema kuwa wanalala bure, hivyo kuna siku atamtimua.

Mbali na hayo akawa anachukua pesa kwa jamaa mmoja wa bodaboda ili amkuwadie dada mmoja mpangaji wenzake.

Kwa dereva wa bodaboda aliendelea kuchukua pesa, huku akimwambia kuwa yule dada amekubali, kumbe si kweli.

Lakini za mwizi arobaini, taratibu waliogombana wakaanza kumjua mbaya wao. Mama mwenye nyumba akaitisha kikao na kila mmoja akaanza kueleza jinsi alivyogombana na mwenzake na tatizo ni nini.

Kila aliyesimama na kuongea, alimtaja moja kwa moja Riyama au mama Tatu kuwa ndiye aliyemwambia maneno hayo.

Dhahiri sasa ikawa yeye ndiye mbea na mgombanishi. Hapo yakaisha. Lakini kumbe wapangaji wa kike wakawa na jambo lao.

Wakaenda kukodisha matarumbeta na 'kigoma cha Uruguay', kwa ajili ya tu ya kumsuta Riyama.

Na kweli lilikua timbwili la aina yake nyumbani hapo.



# HARUFU YA NGOMA 10 MPYA 2024

Na Adam Fungamwango

WASANII wamechafukwa. Ni kama vile mashindano kwani kila mmoja ni kama alikuwa anasubiria mwaka mpya ili atoe ngoma mpya au ashirikishwe.

Baada ya zile ngoma 10 zilizotamba mwaka 2023, zilizotolewa kwa awamu mbili kutokana na mashabiki wengi kupendekeza baadhi ya nyimbo zilizoachwa, leo tumeamua kuweka ngoma 10 mpya ambazo tayari zimeachiwa na wasanii mara tu baada ya 2024 kuingia.

Mpaka sasa katika ngoma zote wasanii wa kiume ndiyo walioonekana kuuchangamkia mwaka mpya, nadhani wa kike bado wanavuta kasi.

**Rayvanny - Down**

Ni kama waliacha kwanza wale mwaka mpya. Tarehe mbili tu, msanii Rayvany akatoa ngoma yake mpya kabisa iitwayo 'Down.'

Ngoma hii ndiyo inayoshikilia rekodi ya kuwa kwanza kabisa ya bongo fleva mwaka huu wa 2024, ikitoka kwa mfumo wa video.

**Roma ft Chid Benz-Nasikia Harufu**

Kesho yake, Januari 3, msanii nguli wa muziki wa hip hop, Roma Mkatoliki, akatoa ngoma yake ya kwanza mwaka huu kwa mfumo wa video, akamshirikisha mkongwe mwenzake, Chidi Benzi, wimbo unaitwa, 'Nasikia Harufu.'

**Diamond Platnumz - I know**

Siku moja baadaye, hiyo ni Januari 4, kama kawaida bwana mkubwa hapitwi na jambo.

Diamond Platnumz, akaibuka na ngoma yake ya kwanza kwa mwaka 2024, iiitwayo,'I Know.' ambayo ipo kwa mtindo wa video.

**Beka Flavour-Missing You Ft Masile**

Siku hiyo hiyo, kama wameambizana, Beka naye akishirikisha Masile akatoa ngoma moja kali, akaiita,' Missing You', ambayo ipo kwenye mfumo wa video. Kumbuka ni Januari 4 hiyo.

**AY ft Ali Kiba ft Joh Makini - Pull Up**

Mkongwe AY, ambaye kwa sasa anajiita AY Masta, akakusanya wakongwe wanzake, Ali Kiba na Joh Makini, akatoa ngoma yake akaiita 'Pull Up', akiitoa Januari 5.

**Ben Pol ft Darassa - My Life**

Bwana mkubwa Ben Pol naye akaona wala isiwe tabu. Na yeye akamwenda mshikaji wake Darasa na kumwambia watoe ngoma yake kipindi hiki hiki ambacho mwaka nado mbishi.

Ilikuwa ni Januari 9, msanii huyo akapandisha ngoma yake mpya, aliyoiita 'My Life.'

**Joh Makini ft Ben Pol - Makasia 'Kilimo Edition'**

Ni siku hiyo hiyo ya Januari 9 ambapo msanii mkongwe Joh Makini alipotoa ngoma yake mpya na ya kwanza mwaka huu, akaiita 'Makasia, Kilimo Edition', na hakuwa peke yake, yeye akaamua kushirikisha Ben Pol.

**Marioo Ft Harmonize - Away**

Marioo naye akaona wala usiwe tabu. Yaani mwaka mpya huu nisitoe ngoma, haiwezekani.

Akaibuka na ngoma yake akishirikisha Harmonize, unaoitwa, 'Away.'

Ilikuwa ni Januari 11 ambapo pini hili lilitoka rasmi na kuanza kuonekana na kusikika kwa watu.

**Dayoo ft Rayvanny-Huu Mwaka**

Dayoo yeye alimfuata Rayvanny na kumwambia akataka kutoa ngoma mpya mwezi Januari na ni lazima aweke 'voko' yake hapo. Na kweli, ngoma ikatoleea Januari 12, ikaitwa,'Huu Mwaka.'

**D Voice ft Lava Lava - Turudiane**

Ngoma zilizidi kumimika mwezi huu wa Januari, D Voice naye akaona wala isiwe kesi, na yeye akamtafuta 'mwanaye', Lavalava na kumwambia wapige kitu chao kipya cha mwaka huu.

Januari 13, wakaifayua ngoma iitwayo, 'Turudiane.'



# Yemi ya nini useme yote?

MWANAMUZIKI mkali kutoka Nigeria, Yemi Alade amesema imekuwa vigumu watu kufahamu asili yake kama yeye anatoka kabila la Yoruba au Igbo.

Akifunguka kuhusu historia yake, amesema makuzi yake yametokana na nyumba ya watu wenye tamaduni mbili tofauti na zinazoheshimika nchini humo.

Yemi ambaye hivi karibuni alialikwa kutumbuiza katika ufunguzi wa michuano ya soka ya mataifa ya Afrika nchini Ivory Coast, amesema baba yake anatoka kabila la Yoruba na mama ni Igbo, hivyo alikuwa katika mazingira ya kufurahisha na yenye kulindwa sawa.

“Sikuwa na ufahamu kuhusu tofauti za makabila hadi baadaye nilipokuwa, hasa wakati watu walipobishana ikiwa mimi ni Yoruba au Igbo, amesema.



## Cynthia wakumbushe uchungu wa mzazi

MWIMBAJI wa Nigeria, Cynthia Morgan, amewajia juu Wanigeria akidai wanamnyanyasa mzee Joseph Aloba ambaye ni baba yake Mohbad.

Cynthia ameandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa baba wa marehemu Mohbad, anaonewa kwa kile anachokipitia katika kulinda mali ya mtoto wake.

Amesema hata kifo cha Mohbad kilikuwa kina utata, lakini Wanigeria wanaungana na mpenzi wa marehemu ambaye anadai haki ya kumiliki mali na kumweka kando baba yake ambaye ana uchungu wa kumpoteza mtoto wake.


## Funke kweli kiboko ya ndoa

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Funke Akindele amesema katika ndoa zote alizopitia, yeye hakuwa sababu ya kuvunjika bali ni wanaume wenyewe.

Akizungumza hivi karibuni, msanii huyo wa filamu za Nigeria, amesema kwamba yeye ana kawaida ya kuchukua hatua pale anapoona ndoa inataka kuanguka, lakini hiyo haina maana amekuwa chanzo.

“Kwangu mimi usiposhindwa huwezi kufanikiwa, lazima uendelee kujaribu lakini unatakiwa kujiinua na kuinuka tena kwangu mimi naona vikwazo ni sehemu ya maisha na sio kushindwa na ukiniuliza ulishindwa kwenye ndoa nitajibu hapana,” amesema.





## Drake amfurahia baba yake

RAPA kutoka nchini Canada, Drake amekuwa na furaha baada ya kuona wazazi wake wanaungana tena baada ya miaka 15,

Kwa miaka mingi, Drake amekuwa akiwatunza wazazi wake kwa usawa, licha ya wote kutenganishwa mipaka ikiwa baba yake yuko Memphis nchini Marekani na mama yake anaishi naye Toronto huko Canada.

Kwa mujibu wa mtandao wa HotNewHipHop, Drake alisaidia zoezi la baba yake kupata kibali kuingia nchini humo na kuungana tena kama familia moja.

## Ayo akumbuka maisha ya utotoni

MWIGIZAJI Ayo Edebiri, amefichua kwamba utoto wake ulitawaliwa na maisha ya misimamo mikali ya kidini.

Akihojiwa na gazeti la The Times la Uingereza, amesema wakati akikua baba na mama yake walikuwa wakizungumzia utii wa dini na maadili yasiyopinda.

Msanii huyo mzaliwa wa Boston Massachusetts, Marekani ameeleza kuwa kama mtoto wa pekee walikuwa wakizungumza naye kama mtu mzima na alikuwa akipenda maisha hayo ambayo anayakumbuka kila siku.





# Hospitali Korogwe rasmi kielektroniki

**Na Oscar Assenga,**
KOROGWE

SHIRIKA la Kimaifa la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) limetoa msaada wa vifaa vya kielektroniki kwa Hospitali ya Mji wa Korogwe mkoani Tanga kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na huduma kwa wagonjwa.

Msaada wa vifaa hivyo ambao umetolewa kwa hospitali hiyo kupitia Wizara ya Afya, utaiwezesha serikali kupata taarifa nyeti za usimamizi wa hospitali za umma nchini, ikiwemo ya Korogwe.

Vifaa hivyo vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ni mahusus kwa ajili ya kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji taarifa za wagonjwa wanaofika hospitalini hapo na utoaji wa huduma za matibabu.

Kaimu Meneja wa Mradi wa Afya GIZ Tanzania, Erick Msoffe, alisema zaidi ya wafanyakazi 150 katika hospitali hiyo wamepatiwa mafunzo ya kutumia mfumo huo wa kielektroniki wa GoTHOMIS kabla ya kufungwa kwa vifaa hivyo ambavyo uwekezaji wake wa awali umegharimu Sh. milioni 200

Kwa mujibu wa Msoffe, ufungaji wa vifaa hivyo umelenga kubadilisha taratibu za kiutawala na kiafya katika hospitali hiyo kwa kuondoa matumizi ya kumbukumbu za karatasi.

Aliyataja malengo mengine kuwa ni kuboresha uhifadhi na upatikanaji wa takwimu za wagonjwa, kuiongeza hospitali ufanisi na kupunguza makosa katika takwimu.

Mkoa wa Tanga una hospitali 18 zinazofadhiliwa na GIZ katika eneo la TEHAMA.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Heri Kilwale, alisema kubadilika kutoka matumizi ya makaratasi hadi mifumo ya kidijitali, kutawasaidia watoa huduma za afya kupata taarifa za mgonjwa kwa wakati na salama.

Alisema pia kutapunguza muda wafanyakazi wa kujaza makaratasi mengi na wataalamu wa afya kupata muda wa kutoa huduma kwa wagonjwa hivyo kuongezeka ubora.

# Wafugaji wazidi kumiminika Handeni

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

KAYA 72 zenye watu 515 na mifugo 2,206 zimehama kwenye ardhi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na kwenda kuanza maisha mapya katika kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga.

Maeneo mengine yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya wanaohama kwa hiari Ngorongoro ni kijiji cha Kitwai kilichoko Simanjiro mkoani Manyara na kijiji cha Saunyi, Kilindi mkoani Tanga.

Akizungumza juzi wakati wa kuwaaga wafugaji hao, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Richard Kiiza, alisema kundi hilo ni kubwa kuliko mengine yaliyotangulia kuondoka kwa hiyari katika eneo hilo la hifadhi baada ya kujiandikisha.

Kwa mujibu wa Kamishna Kiiza, hadi sasa zaidi ya kaya 1,070 zimejiandikisha kuhama katika eneo hilo kwa hiari. "Kadri ujenzi wa nyumba za makazi unavyoendelea kukamilika katika vijiji vya Msomera, Kitwai na Saunyi, idadi ya wananchi wanaojiandikisha nayo inaendelea kuongezeka. Mpaka sasa tuna kaya 1,070 zilizojiandikisha zikisubiri kuondoka kwa hiari. "Kazi ya ujenzi wa nyumba 5,000 Msomera, Saunyi na Kitwai inaendeela chini ya SUMA JKT (Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa) na tayari zaidi ya nyumba 360 zimekamilika na nyingine zaidi ya 2,000 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi," alisema.

Awali, Meneja wa Mradi wa Kuhamisha Wananchi Waishio ndani ya NCAA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Fedes Mdala, alisema kuhama kwa kundi hilo kunafikisha kaya 749 zenye watu 4,337 na mifugo 19,915 kuondoka katika hifadhi hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kanali Wilson Sakulo, alisema haki za binadamu zimezingatiwa ikiwa ni pamoja na kulipwa stahiki zote za msingi kwa wananchi wanaohama kwa hiyari katika hifadhi hiyo.

Baada ya hapo, wananchi hao wanapatiwa nyumba yenye hati kwenye eneo la ukubwa wa ekari 2.5, shamba ekari tano, huduma za maji, shule, afya, barabara, mabwawa, majosho, minada, umeme na mawasiliano.



Muuguzi Daraja la Pili katika Kitengo cha Endoscopia Hospitali ya Rufani ya Mount Meru, Ruth Lijimbe (kushoto), akitoa maelezo kuhusu kifaa cha kuchunguza magonjwa ya tumbo kwa maofisa kutoka Wizara ya Afya, TAMISEMI na waandishi wa habari wanaotembelea kukagua miradi ya afya iliyopata fedha za mfuko wa pamoja wa afya ya msingi, mkoani Arusha, jana. Kulia ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Charles Mkombachepa. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Posta yajikita biashara mtandao

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

POSTAMASTA Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Maharage Chande, amesema shirika hilo linaendelea kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kufanya biashara mtandao ili kukidhi ushindani wa bidhaa katika ukanda wa Afrika na Dunia.

Akizungumza jana wakati wa Maadhimisho ya Miaka 44 ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU), Chande alisema shirika hilo kwa sasa linafanya mabadiliko makubwa ya kuboresha huduma ili kuendana na kasi ya teknolojia ambayo inakua kwa kasi duniani.

"Tunatekeleza sera na mipango ya nchi katika kukuza biashara mtandao ambayo inajumuisha usafirishaji wa vipeto kwa njia ya haraka ambapo tumeshafungua vituo vya utimilifu Arusha, Zanzibar, Dodoma na Dar es Salaam ili ndani ya siku mbili mtu akiwa sehemu yoyote duniani anapokea mzigo wake," alisema.

"Miaka 10 iliyopita tulikuwa tunafanya bajeti kubwa ya uuzaji wa ndani ya mabango makubwa ili tuwafikie wateja wengi wanaotumia zaidi huduma zetu, lakini leo mambo yamebadilika tukitumia tweet moja tu inawafikia mamilioni ya watu kwa hiyo na sisi Shirika la Posta lazima tubadilike kulingana na mabadiliko ya kidijitali yanayoikumba Dunia nzima," alisema.

Alisema wanampango wa kutengeneza mfumo wa kuwawezesha wananchi kuhuhisha vivambulisho vyao mbalimbali, zikiwemo hati za kusafiria na vya uraia (NIDA) na vingine vitakavyokuwa vinatambulika kwa wakati huo.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Celestine Kakele, alisema wanajivunia kama nchi kutimiza ndoto ya waasisi wa Afrika kwa kuwezesha upatikanaji wa jengo hilo la makao makuu ya PAPU barani humo.

"Kutekeleza majukumu ya kisera na kibiashara katika mashirika ya posta kwa nchi za Afrika ni jambo muhimu, lakini kuna mambo chanya yanayoathiri utoaji wa huduma ambayo ni lazima twende na wakati kwa kuwekeza kwa kasi ili tusiachwe na teknolojia na utoaji huduma ya kibiashara kwa njia ya mtandao," alisema.

Alisema serikali inajikita katika kuweka mikakati kuhusu teknolojia za muundo wa biashara mtandao ili kuhudumia wananchi wengi zaidi.

"Nawapongeza Shirka la Posta kwa hatua mliopiga katika kujiendesha kidijitali ikiwemo usafirishaji wa vipeto maeneo mbalimbali Afrika na duniani," alisema.

Waziri wa Habari, Mawasiliano Teknolojia na Posta wa Zimbabwe, Dk. Tatenda Mavetera, alisisitiza PAPU kuweka mikakati thabiti inayoendana na kasi ya kidijitali kuvuta zaidi wafanyabiashara kutumia huduma zao.

"Tunataka kuona PAPU inasonga mbele katika uwekezaji wa posta ya kidijitali na kukuza biashara mtandao katika ukanda wa Afrika.

"Nikiwa Mwenyekiti wa Mipango ya Mawaziri wa masuala ya Posta nataka kuwahakikishia mipango yetu yote tunayojiwekea inatekelezeka kwa wakati, " alisema.

Alisema uongozi wa juu wa umoja huo utahakikisha shirika la posta linaendelea kukua barani Afrika kwa kasi kwa kuimarisha mawasiliano na miundombinu ya kidijitali.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# IVORY COAST BAADA YA MIAKA 40

## AFCON ile matokeo redioni siku ya pili, sasa ni 'laivu'

**Na Adam Fungamwango**

MPIRA. Timu ya taifa ya Cameroon imefanikiwa kutwaa Kombe la Mataifa Huru Barani Afrika kwa kuifunga timu ya taifa ya Nigeria mabao 3-1 katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny, Abidjan nchini Ivory Coast.

Mabao ya Cameroon yamefungwa na Rene Brice N'Djeya dakika ya 32, Theophile Abega dakika ya 79 na Ernest-Lottin Ebongue dakika ya 84, na la Nigeria ambao walitangulia kufunga dakika ya 10 ya mchezo lilifungwa na Garba Lawal."

Ilikuwa ni sauti ya mtangazaji wa Taarifa ya Habari ya Radio Tanzania Dar es Salaam. Ilikuwa ni siku moja baada ya mechi hiyo kuchezwa.

Mechi hiyo ilichezwa Machi 18, 1984 ambapo fainali hizo zilichezwa nchini Ivory Coast.



Mechi ya fainali kati ya Cameroon iliyoshinda mabao 3-1 dhidi ya Nigeria mwaka 1984 na kutwaa kombe, katika AFCON iliyopigwa nchini Ivory Coast, ambapo mwaka huu imeandaliwa nchini humo baada ya miaka 40.

Matokeo yakatangazwa kwenye Taarifa ya Habari kesho yake Machi 19, michuano hiyo inafanyika tena kwenye ardhi hiyo ikiwa ni miaka 40 imepita, tangu wakati huo likiitwa Kombe la Mataifa Huru mpaka sasa ambapo inajulikana kama michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Ilikuwa ikiitwa hivyo wakati huo kwa sasa si nchi zote Afrika zilikuwa huru. Zingine bado zilikuwa zinatawaliwa, na hivyo zilitengwa kwa ajili ya kuwaonyesha waliokuwa wakizitawala kuwa hawaungi mkono jambo hilo.

Dunia inakwenda kasi sana. Wakati mwingine ukikaa peke yako huwezi kuamini kama baada 40 kupita kila kila kitu kimebadilika.

Ukiwahadithia vijana wa kizazi cha sasa wanaweza kukuona unawaongopea, na wale ambao watakuamini baadhi wataangua vicheko na wengine kukuonea huruma.

Ukiwaambia kuwa zamani matokeo ya mechi za Mataifa ya Afrika, AFCON yalikuwa yakipatikana baada ya siku mmoja kupita, hapo yatatangazwa redioni, lakini kwenye gazeti ni baada ya siku mbili, watashangaa. Lakini ukweli ndivyo ulivyo.

Huo nilioutoa juu ni mfano hai wa mechi hiyo ya fainali ambayo yenyewe kwa sababu ilikuwa fainali ilitangazwa kwenye taarifa ya habari, Redio Tanzania Dar es Salaam.

Kwa nini taarifa ya habari, kwa sababu stori hiyo ni kubwa. Ni stori ya fainali ya Mataifa Huru Barani Afrika.



Mashabiki wa soka zamani wakisikiliza matokeo ya mechi za AFCON kwa kutumia redio, baada ya siku moja kupita.

Na siyo hiyo, hata bingwa wa Klabu Bingwa Afrika alikuwa anatangazwa kwenye taarifa ya habari.

Lakini matokeo ya mechi hizi za kawaida tunazoiona zinaendelea, hutangazwa kwenye vipindi vya michezo, saa mbili kasorobo.

Vile vile hutangazwa kwenye redio siku moja baada ya mechi na siku ya pili kwenye gazeti.

Mfano mechi ikichezwa Jumapili, basi hapa Bongo hakuna anayejua matokeo mpaka kesho yake Jumatatu usiku saa mbili kasorobo kwenye kipindi cha michezo ndipo itakapojulikana kama mechi iliyochezwa jana nani alishinda. Na Jumanne ndiyo utaamkia nayo gazeti.

Pamoja na kwamba tatizo hakukuwa na mitandao ya kijamii, lakini Tanzania pia haikuwa na televisheni kama baadhi ya nchi za Kiafrika.

Baadhi ya nchi za Kiafrika zilikuwa na stesheni ya televisheni hivyo ziliweza kuangalia mechi hizo moja kwa moja, lakini Bongo ilikuwa ni giza tupu.

Leo hii mambo ni tofauti. Unaangalia watoto zako, mkeo sebuleni wakiangalia mechi laivu, yaani inaonyeshwa moja kwa moja muda ule ule wanaoangalia unaona wakati mwingine kama miujiza.

Halafu ukifikiria kipindi kile ambacho wakati mwingine hata hiyo redio tu haipo kwa watu wote na wewe ulilazimika kwenda kusikiliza kwa jirani, unaona kweli kuna maendeleo nchini.

Leo hii kwenye vibanda umiza na majumbani watu wanakaa kuangalia mechi za AFCON, kuangalia timu yao ya taifa la Tanzania ikicheza laivu ni maendelea makubwa sana.

Ni tofauti na fainali kwa kwanza mwaka 1980, iliyochezwa nchini Nigeria hakuna yoyote wakati huo aliyepata bahati ya kuiangalia laivu.

Watanzania walikuwa wanapata matokeo tu kupotia kipindi cha michezo, na timu ikitwaa ubingwa siku hiyo inapata bahati stori hiyo inasomwa kwenye taarifa ya habari.

Leo ni miaka 40 kamili tangu Ivory Coast ilipoandaa michuano ya AFCON 1984, likichukuliwa na Cameroon kwa kuifunga Nigeria mabao 3-1, wakati ule matokeo tulikuwa tunasikiliza kwenye redio, leo tunaangalia laivu kwenye televisheni ni jambo la kushukuru hasa kwa kizazi ambacho kimepitia mapito hayo na leo kinashuhudia mabadiliko makubwa ya kiteknolojia.

Ni somo pia kwa kizazi cha sasa kuwa nchi hii imetoka mbali sana na sasa imepiga hatua kubwa kimaendeleo

**Tuma meseji 0716 350534**



Mashabiki wa soka wa sasa wakishangilia na kuangalia laivu mechi za AFCON moja kwa moja ikichezwa muda huo huo kutoka nchi husika iliyoandaa fainali hizo.

HABARI KIMATAIFA

# Israel yasisitiza hakuna taifa huru la Palestina

**TEL AVIV,** ISRAEL

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema ameitaarifu Marekani kwamba anapinga kuanzishwa kwa taifa huru la Palestina baada ya kumalizika vita.

Katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jana, Netanyahu alisisitiza nchi yake itaendelea na mashambulizi katika Ukanda wa Gaza hadi ushindi kamili utakapopatikana.

Alisema ushindi huo utaambatana na kutokomezwa kwa kundi la Hamas na kurudishwa mateka walisalia wa Israeli.

Netanyahu alieleza mafanikio hayo yanaweza kupatikana baada ya miezi zaidi.

Vita hiyo imesababisha vifo vya Wapalestina 25,000 katika eneo la Ukanda wa Gaza huku asilimia 85 ya wakazi wake wamekimbia makazi yao.

Hata hivyo, Israel iko katika shinikizo la kudhibiti mashambulizi yake na kushiriki katika mazungumzo ya kukomesha mapigano hayo.

Washirika wa Israel, ikiwamo Marekani wamehimiza kufufuliwa kwa mazungumzo ya kutafuta suluhu ya muda mrefu ili kuundwa kwa taifa la Palestina litakalopakana na Israeli.

Matumaini ya mataifa mengi ni kuona pande zinazozozana kurudi kwenye meza ya mazungumzo kama njia pekee inayowezesha kupata suluhu ya kudumu.

Lakini kutokana na maoni ya Netanyahu, inaonekana nia yake ipo kinyume na matarajio ya wengi.

Katika mkutano huo, waziri mkuu huyo alisema Israel lazima iwe na udhibiti wa usalama katika ardhi yote ya magharibi mwa Mto Jordan, ambayo itajumuisha eneo la taifa lolote la baadaye la Palestina.

"Hili ni sharti la lazima, na linapingana na wazo la mamlaka ya Palestina. Nini cha kufanya? Ninawaambia ukweli huu marafiki zetu wa Marekani, na pia nilisimamisha jaribio la kuweka ukweli juu yetu ambao ungeweza kudhuru usalama wa Israeli, " alisema.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Israel limezidisha mashambulizi yake dhidi ya mji wa Khan Yunis ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Katika mashambulizi hayo yaliyofanyika alfajiri ya Ijumaa, yalihusisha ndege za kivita na mizinga iliyolenga maeneo mbalimbali ya mji huo.

Shirika la Habari la Palestina lilisema kuwa takriban watu wanne waliuawa wakati wa shambulio la bomu lililolenga nyumba moja katika eneo la magharibi la Khan Yunis, huku shambulio lingine la anga likilipua vizuizi vilivyowekwa kwenye nyumba za makazi.

Shirika hilo lilieleza kuwa jeshi la Israel lililenga maeneo ya karibu ya Hospitali ya Al-Amal katika mji huo kwa mashambulio ya mizinga mikubwa na risasi.

Pia mashambulizi hayo hayakunusuru eneo la katikati ya mji huo kwa kupigwa mabomu yaliyoharibu nyumba na miundombinu ya barabara.

**BBC**



Wingu la moshi likitanda juu ya anga la mji wa Khan Yunis ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza baada ya vikosi vya Israel kushambulia kwa mabomu jana. **PICHA: REUTERS**

# Mahakama Kenya yaruhusu kuanzishwa bima mpya ya afya

**NAIROBI,** KENYA

MAHAKAMA ya rufani nchini Kenya, imeruhusu utekelezaji wa sheria mpya ya bima mpya ya afya baada ya Mahakama Kuu kusitisha kutokana na sababu mbalimbali.

Wakitoa hukumu hiyo jana, majaji Patrick Kiage, Pauline Nyamweya na Grace Ngenye walisema kutokana na kusitishwa kwa uanzishwaji wa mfuko huo wa afya, kuna hatari ya raia wengi ambao sio wahusika katika kesi inayosubiri hukumu katika mahakama zingine kukosa haki ya kulinda afya zao.

"Tunashawishika kuwa mkanganyiko, hatari na madhara kwa wananchi wanaosubiri kusikilizwa na kuamuliwa kwa rufaa hiyo ni suala gumu kwa waathiriwa, itakuwa na athari ya kuifanya rufaa kuonekana vibaya," zilisema hati za mahakama.

"Tunasitisha amri za Mahakama Kuu zinazozuia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya ya Jamii ya 2023, Sheria ya Huduma ya Afya ya Msingi ya 2023 na Sheria ya Afya ya Kidijitali ya 2023...," walisema majaji hao.

Hata hivyo, Kifungu cha 26(5) cha Sheria kinaweka usajili na mchango kuwa sharti la awali la kushughulikia au kupata huduma za umma kutoka kwa serikali ya kitaifa na kaunti au vyombo vyake na Kifungu cha 27(4) ambacho kinatamka kwamba mtu atapata huduma za afya pale tu michango yao kwenye Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii inasimamishwa.

Wahusika katika kesi hiyo wamepewa muda wa siku saba kuwasilisha pingamizi la kimaandishi kuhusu vifungu vitatu vya sheria ya bima ya afya ya jamii ambavyo vimesimamishwa.

Msajili wa mahakama ya rufaa baada ya hukumu hiyo atapanga tarehe ya kusikilizwa kwa kesi hiyo kabla ya Machi 3, mwaka huu.

Waziri wa Afya, Susan Nakhumicha ambaye alikwenda mahakamani hapo alisema uamuzi wa Mahakama Kuu ulisababisha Wakenya wengi kunyimwa huduma ya matibabu kulingana na katiba ya nchi hiyo.

**BBC**

## Pakistani wajifungia kuijadili Iran

**ISALAMABAD,** PAKISTAN

WAZIRI Mkuu wa Pakistan, Anwar-ul-Haq Kakar, ameitisha mkutano wa dharura na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kujadili msuguano kati ya nchi yake na taifa jirani la Iran.

Waziri wa Habari wa Pakistan Murtaza Solangi, alisema mkutano huo ulifanyika jana baada ya nchi hizo mbili kushambuliana kwa kutumia ndege zisizo na rubani na makombora.

Kulingana na Solangi, mkutano huo ulijadili maslahi mapana ya usalama wa taifa hilo katika kudhibiti mashambulizi ya Iran.

Umoja wa Mataifa na Marekani zimehimiza nchi hizo kuwa na uvumilivu, wakati nchi ya China ikijitolea kuwa mpatanishi katika mzozo huo.

Ofisa wa usalama wa Pakistan alieleza kwamba mkuu wa majeshi na mkuu wa idara za upelelezi walihudhuria mkutano huo.

Waziri Mkuu Kakar juzi alikatisha ziara yake kuelekea Davos nchini Uswisi kuhudhuria mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani.

**DW**

## Tshisekedi kuapishwa leo, upinzani walegeza msimamo

WAKATI Rais Felix Tshisekedi anaapishwa leo kuendelea na nafasi hiyo kwa muhula wa pili, viongozi wa vyama vya upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wamesitisha maandamano nchi nzima.

Wagombea hao Moise Katumbi, Martin Fayulu, na Floribert Anzuluni, badala yake wamewataka wafuasi wao kuelezea kutoridhika kwa kusimama na kusema hapana katika maeneo yote ya nchi hiyo.

Rais Felix Tshisekedi anatarajiwa kuapishwa kushika nafasi hiyo kwa muhula wa pili katika sherehe itakayofanyika mjini Kinshasa.

Akizunguza na wanahabari, Fayulu alisema wameamua kusitisha maandamano hayo kwa sababu hawawezi kuwapeleka watu wakauwawe.

Alisema Wakongo wote wanajua kuwa uchaguzi huo ulikuwa sawa na mchezo wa kuigiza.

Desemba 27 mwaka jana, upinzani uliitisha maandamano ambayo yalipigwa marufuku na mamlaka ya nchi hiyo.

Rais Tshisekedi alishinda katika uchaguzi mkuu uliofanyika Desemba 20, mwaka jana kwa kupata asilimia 73.27 ya kura zote.



Rais Felix Tshisekedi

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**Aminiel Richard Mnkeni** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.358/0060** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SHIGHATINI SEKONDARI mwaka 1994. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **KLR/RB/1539/2012**

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

By this **DEED I DAMAS KARLO LUENA of P.O.BOX 82, SONGEA** do hereby absolutely renounce and abandon the use of name **OF THOMAS KARU** and in lieu thereof do assume and adopt this 2nd day of **JANUARY2024** the name of **DAMAS KARLO LUENA.**

**AND IN PUSUANCE** of such change of name as aforesaid, **I HEREBY DECLARE** that I shall at all times hereafter, in all records, deeds and instruments in writing and in all dealings and transactions and upon alloccasions whatscever , use and sign the said name of **DAMAS KARLO LUENA** as my name in lieu of the said name of **THOMAS KARU.**

**AND I HEREBY AUTHORISE** and request at designate and address me in the name of **DAMAS KARLO LUENA** only.

**IN WITNESS WHEREOF I** have here to subscribed my name of **DAMAS KARLO LUENA.**



**Signed and DELIVERED at Songea by the said DAMAS KARLO LUENA Known to me personally this 2nd day of,.......... January 2024**

DEPONENT

**NAME :** **GASTON MAPUNDA**
**SIGNATURE:** ............................
**POSTAL ADDRESS :** **997 SONGEA**
**QUALIFIFICATION:** **STATE ATTORNEY**
**COMMISIONER FOR OATH**



## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NICHOLAS DOMINIC FRANCIS** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI, GARI LENYE NAMBA ZA USAJILI **T 530 DPQ** AINA YA **TOYOTA RAV 4** ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **MAS/RB/TR/02/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **SIMBA YUSUFU SIMBA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T566 EBC**. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/520/2024.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **RAMADHANI HAMEDI RASHIDI** amepotelewa na kadi ya gari lenye namba za usajili **T931 DBP.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/MUL/558/2024.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

## KUPOTEA KWA VYETI



**MIRIAMU PETRO NG'ENI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index **No.S1861/0012/2017** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MERYA SECONDARY SCHOO**L mwaka 2017, Cheti cha kidato cha sita chenye **No.S0281/0654/2020** kilichotelewa na CHIEF IHUNYO GIRLS HIGH SCHOOL mwaka 2020.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/11137/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YASIN MOHAMED ALLY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA PREMIO YENYE USAJILI **T621 BEV** CHASISI NAMBA **AT2100016000,**ENGINE NAMBA **4AL885639** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/239/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDWARD PETER MASHINGIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina Ya **BACKHOE LOADER** yenye jina la umiliki **MASCONS TANZANIA LIMITED** yenye usajili namba **T.978 DMH,** CHASSIS NAMBA: **CAT0426FCEJ400293** na ENGINE NAMBA: **CC200642.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/8789/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILLIAM TIBAKYETA MAGENZI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 740 DDB,** CHASSIS NAMBA: **SR400160155** na ENGINE NAMBA: **3S5029283.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/1409/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 686 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE TALUMBA MAIKO TALUMBA**


**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**
**NEEMA ALEX LIBONGI**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 13 day of 02/2024

DATED at MOROGORO this 19TH day of 01 2024




## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI JKT SUMA JKT** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta , yenye namba za usajili **T 722 CER** Yenye Chassis Namba **T 2184710,** Engine Namba **E2187660** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa : **PHQ/KIL/MOS/1129/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUSANI VICTORY NDENDYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 134 DNP, CHASSIS** NAMBA: **SR400207461** na ENGINE NAMBA : **3SFE924Z852DM.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MKO/TR/RB/09/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE MICHAEL WAKUGANDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye usajili namba **T998 DVY.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CEN/RB/27010/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CLIFFORD STEVEN NZALI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NISSAN SAFARI YENYE USAJILI **T900 AJK** CHASISI NAMBA **WYY60610215,** ENGINE NAMBA **RO23426421X** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/739/2024.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi.
Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa.
Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.
Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Mama mwenye nyumba-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu.

Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa.

Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba.

Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu.

Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

*************************************




Kundi zima lilifika kwenye nyumba hiyo inayosemekana kuwa msichana yupo ndani na mume wa mtu.

"Kwani wewe msichana upo na nani humo?" Yule mzee ambaye alikuwa anakaa nyumba jirani akauliza.

"Niko peke yangu, mimi nimeachiwa chumba na shoga yangu Zai, yeye amekwenda msibani, sasa huyu mama na wenzake na umati wote huu umetoka huko umevamia hapa unasema mimi nimechukua mume wa mtu!" Mwadawa alijibu akiwa dirishani.

"Sasa mbona umejifungia kama hakuna mtu humo ndani?" Akauliza tena mzee huyo.

"Nimejifungia kwa sababu ya usalama wangu wala siko na mwanaume humu ndani. Yaani kundi lote hilo wanataka kunivamia mimi wanipige!"

"Unawafahamu hawa waliokuja?"

"Huyo dada anayesema mumewe yumo humu na wenzake ni wapangaji na mama yangu, kila siku nyumbani ugomvi, leo wamenifuata huku wananituhumu niko na mume wao, jamani." Mwadawa alizidi kukana akiwa chumbani, mlango ukiwa umefungwa na alikuwa anazungumza kupitia dirishani.

"Mimi sina, ninachotaka afungue tu mlango nihakikishe yumo au hayumo." Devota aliongea kwa hasira.

"Hapana mama, mlango hauwezi kufunguliwa hivi, watu wote hawa waliojazana nje, hapa tutakachofanya ni kutuma watu kwenda Serikali za Mitaa na kwa mjumbe ili waje na kama jambo hili lipo, basi taratibu zifuatwe bila kuvunjwa taratibu na sheria wala uvunjifu wa amani.

**"Huyo dada anayesema mumewe yumo humu na wenzake ni wapangaji na mama yangu, kila siku nyumbani ugomvi, leo wamenifuata huku wananituhumu niko na mume wao, jamani." Mwadawa alizidi kukana akiwa chumbani, mlango ukiwa umefungwa na alikuwa anazungumza kupitia dirishani.**

"Jamani eee, yupo mume wa mtu yupo hayupooo" Mtu mmoja alipaza sauti na kufuatiwa na kelele za kushangilia kutoka kwa umati uliokuwepo uliokua unatishia pia amani.

Umati ule ulikuwa uko pale kwa ajili ya jambo moja tu. Kushuhudia fumanizi na si kitu kingine.

Na kila muda ulivyokuwa unazidi kwenda ndivyo watu walivyozidi kumiminika. Ina maana walikuwa wanaambizana mitaani.

Haukupita muda mrefu walifika watu watatu, Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa, Mjumbe na mtu mmoja ambaye ni Polisi Jamii.

Mwenyekiti alisimama katikati ya umati uliokuwa umemzunguka na kuanza kuongea kwa mamlaka aliyokuwa nayo.

"Jamani naomba mnisikize, mimi kama mwenyekiti wenu nimefika hapa, tulikuwa kwenye ofisi za kata tukapata taarifa hizi. Tumekuja hapa siyo kukoleza ugomvi, au fumanizi kama tulivyosikia, lakini sisi kama viongozi na walinda usalama tumekuja hapa kuhakikisha kama ni kweli wapo au yupo huyo mtu anayetuhumiwa ili tuwachukue na kuwapeleka sehemu ya usalama.

Tumekuja na Polisi Jamii hapa ili kama kweli lipo hili wahusika wasiguswe na mtu yeyote wafikishwe sehemu na kama kuna mengine taratibu zitafuata baada ya hapo," alisema, lakini pia kwa pembeni kukiwa na sauti zilihanikiza, "Watoe, watoe, watoe."

Baada ya mashauriano ya dakika tano hivyo, iliamriwa mlango ufunguliwe.

Wa kwanza kuingia alikuwa ni mjumbe wa nyumba kumi, ambaye alitumia dakika tano kuingia chumbani humo na akatoka.

Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa akawa wa pili, naye akaingia peke yake, akatumia dakika nne na sekunde kadhaa, naye akatoka.

Wa mwisho kuingia alikuwa ni Polisi Jamii. Yeye akatumia kama dakika saba hivi.

Akatoka nje. Hakuwa peke yake. Mkononi alikuwa amemshika mwanaume mmoja mwenye umri unaokadiriwa kufikia au kukaribia miaka 30 hivi, aliyevaa shati jeupe na suruali ya jeans nyeusi na viatu aina ya raba rangi ya bluu.

Ile kutoka tu, umati ulipiga kelele ambazo zilikuwa za aina tofauti. Wengine walikuwa wanashangilia na wengine kuzomea. Zote zilitoka kwa wakati mmoja na kusababisha kelele zisizokuwa na mpangilio.

Kwanza zilizuka vurumai, Devota akitaka kwenda kumpiga mumewe, lakini alidhibitiwa na askari.

"Mama ndiyo huyu mumeo?" Akauliza Mwenyekiti wa Serikali ya Mitaa Magomeni Mikumi.

"Ndiyo, na anatembea na binti wa mama mwenye nyumba yangu, kuwadi ni mama yake mwenyewe."

"Mbona hammtoi huyo fisadi kiwembe mchukua waume za watu?" Akapiga kelele Tabia, mpangaji mwenzake Devota.

Na hilo ndilo kama lilikuwa swali la wengi, ambao walitaka msichana aliyekuwa naye mle nadhani naye atolewe, wote wapelekwe kituoni.

"Sisi tunaiwakilisha serikali, mle ndani yule binti ametuambia amechiwa chumba na rafiki yake ambaye amekwenda kwenye msiba wa mama yake mdogo.

Ndugu wananchi tunachofanya hapa ni kumchukua huyu bwana kwa usalama wake, tunampeleka sehemu ya usalama kwa sababu bado kuna watu wana hasira naye akiwemo mkewe.

Binti yeye siyo kama tumemuacha, ila kwa busara tumeona tumuachie aendelee kulinda chumba cha mwenzake, kwa sababu kama tukimchukua halafu kukatokea kitu chochote kibaya, ikiwemo wizi, ataingia kwenye matatizo wakati ana matatizo mengine. Tumemuacha kwa muda, akirudi mwenzake tumemwambia aripoti kwanza kituoni, mengine yatafuata baadaye." Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa alitoa ufafanuzi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SERENGETI GIRLS YAANZA KUJINOA KUIVAA ZAMBIA

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 25 cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kimeingia kambini leo jijini, Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa kufuzu Fainali za Kombe la Dunia dhidi ya yosso wenzao kutoka Zambia.

Mechi ya kwanza kati ya Serengeti Girls dhidi ya Zambia itachezwa Februari 2, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, alisema kikosi chake kinaanza maandalizi mapema kwa sababu wanahitaji kupata matokeo mazuri dhidi ya wapinzani wao kwa sababu anatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu.

Shime alisema mechi hiyo pia itakuwa na ushindani mkubwa kutokana na ubora wa wapinzani wao lakini anaamini maandalizi watakayofanya yatawaweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo ya kusonga mbele.

"Tunaingia kambini leo (jana), kwa ajili ya kujiandaa vizuri kuwakabili Zambia, ninaimani tukijiandaa vizuri tutafanya vyema kwa sababu matarajio yangu ni kuona tunasonga mbele katika michuano hii muhimu," alisema Shime.

Kocha huyo aliongeza programu yake ya awali ni kufanya mazoezi yatakayokuwa na mbinu tofauti tofauti na pia kucheza michezo ya kirafiki ambayo itapatikana kupitia maombi yaliyofanywa na viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

„Baada ya mazoezi, pia katika programu yangu nimeomba kupata mechi za kirafiki ili kujiweka imara zaidi, TFF imeshaanza kufanyia kazi, tunaamini hakutakuwa na mchezo rahisi, ndio maana tutahitaji kuwa imara," Shime alisema.

Aliwataja wachezaji walioingia kambini jana ni pamoja na makipa ni Marian Shaban, Mwanaidi Maulid (Bunda Queens), Salome Saint (Geita Gold Queens) wakati mabeki ni Sarah Joel, Manka Richard (Fountain Gate Princess), Neema Damas (Baobab Queens), Edna Makamba (Oysterbay Queens), Ladia Maximilian (JKT Queens), Masika Mwakisua (Yanga Princess), Sarah Lucas na Kulwa Rockets wa Bunda Queens.

Viungo ni Winifred John (Yanga Princess), Ester Maseke, Melikia William, Semeni Juma (Bunda Queens), Naomi Charles, Sabina Alex, Asha Ramadhani (Geita Gold Queens) na Marry Siyame (Laliga Academy- Hispania wakati washambuliaji ni Jamila Rajabu, Yasinta Mitoga, Winifrida Gerald, Mwantima Mwarabu (Geita Gold Queens) na Jamila Celestine wa Bunda Queens.



Mashabiki wakifurahia wakati wa mechi ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), kati ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), dhidi ya Morocco iliyochezwa Jumatano iliyopita. Mashabiki hao waliangalia mechi hiyo pamoja kupitia uzinduzi wa Kampeni ya Soka Live na betPawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# betPawa yanogesha AFCON Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kesho itaikabili Zambia, Kampuni ya michezo ya kubahatisha ya betPawa imenogesha Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) yanayoendelea Ivory Coast kwa kumwaga zawadi mbalimbali kwa mashabiki.

Kampuni hiyo kwa sasa inaendesha kampeni "Soka Live na betPawa" ambapo mbali ya kuwakutanisha mashabiki kuangalia mpira pamoja, hutoa zawadi mbalimbali kama jezi, mabegi, mipira, vikombe na chupa za maji.

Uzinduzi wa kampeni hiyo ulifanyika kwenye baa ya Kitambaa Cheupe, Dar es Salaam ambapo mashabiki walipata fursa ya kuangalia mubashara mechi kati ya Stars dhidi ya Morocco ambapo Tanzania ilifungwa mabao 3-0.

"Soka ni mchezo unaounganisha furaha na hasa pale mashabiki wanapojumuika pamoja. Hii ndiyo sababu tuliona inafaa betPawa kwa kushirikiana na Startimes kuendesha kampeni hii ili kuwafanya mashabiki kuishangilia Taifa Stars wakiwa na ari moja,"alisema Meneja Masoko wa betPawa Tanzania, Borah Ndanyungu.

Alisema kampeni hiyo itaendelea kesho kwenye Ukumbi wa Juliana Pub, Mbezi wakati Stars itakapovaana na Zambia.

Zaidi ya mashabiki 300 walihudhuria hafla hiyo ambayo pia iliambatana burudani mbalimbali.

## Mnali, Daniela pigo kwa Simba Queens

**Na Saada Akida**

MABEKI tegemeo wa Simba Queens, Diana Mnali na Daniela Ngoyi hawatakuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa Bunda Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Karume, Musoma, imefahamika.

Taarifa kutoka Simba Queens zinasema mabeki hao wameachwa katika msafara ulioondoka Dar es Salaam kuelekea Bunda jana kutokana na majeraha ya goti yanayowakabili.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa timu hiyo, Seleman Makanya alisema mabeki hao walikuwa katika mipango ya mechi hiyo lakini wameondolewa na watakuwa nje ya uwanja wa muda wa wiki mbili.

„Kikosi chetu kimeondokana leo (jana) na tumeenda (Bunda) mapema kwa ajili ya kuzoea mazingira, wachezaji wote wako vizuri na tunaenda Mara kwa ajili ya kutafuta alama tatu muhimu dhidi ya Bunda Queens, ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa kufanya vizuri katika ligi," alisema Makanya.

## JKT kusajili vifaa, yawaza makubwa

**Na Oliver Albert**

WAKATI mabingwa wa kikapu Tanzania (NBL), JKT wataanza mazoezi keshokutwa ili kujiandaa na Ligi ya Mkoa wa Da res Salaam (RBA), klabu hiyo imepanga kusajili wachezaji wenye viwango vya juu kwa ajili ya kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa.

JKT imepania kufanya vizuri na kufuzu michuano ya Ligi ya Kikapu Afrika (BAL) ambayo wao ni wawakilishi wa Tanzania katika michuano hiyo.

Kocha wa JKT, Christian Jacob 'Webber' aliliambia Nipashe jana wanataka kusajili nyota wenye uzoefu na watakaowasaidia kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali yanayowakabili msimu huu.

"Msimu uliopita tulikosa ubingwa wa RBA kwa sababu hatukuwa na mzunguko mzuri wa wachezaji tofauti na wenzetu (Dar City). Tulikuwa hatuna wigo mpana katika bechi letu, wenzetu kila mchezaji aliyekuwa anaingia alikuwa na nguvu ile ile tofauti na sisi," alisema Webber.

Aliongeza anafahamu michuano ya kimataifa ni migumu na wamejifunza kutokana na makosa huku akiamini siku moja Tanzania itatwaa ubingwa wa mashindano ya Ligi ya Afrika.

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE, LINDELOF SOKONI

MANCHESTER United inafikiria kurekebisha safu yao ya ulinzi katika msimu wa joto jambo ambalo linaweza kumaanisha beki wa kati Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30, na mlinzi wa Sweden, Victor Lindelof (29) kuondoka ikiwa ofa muhimu zitatolewa kwa ajili yao. **(ESPN)**

### ANDRE ANUKIA FULHAM

KLABU ya Fulham imewasilisha ombi la pauni milioni 30 pamoja na nyongeza ya pauni milioni tano kwa ajili ya kiungo wa Fluminense, Andre mwenye umri wa miaka 22, huku wakiwa tayari wamekubaliana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. **(Ben Jacobs)**

### GYOKERES ATAJWA CHELSEA

KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, amesema Chelsea italazimika kuanzisha kipengele cha kutolewa cha euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres, ikiwa wanataka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. **(Goal)**

### PHILLIPS SAFI WEST HAM

WEST Ham ni moja ya klabu zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Manchester City, Kalvin Phillips na wagonga nyundo hao wapo katika nafasi nzuri ya kushinda katika kinyang'anyiro cha kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 28. **(Standard)**

### PORRO KUREJEA CITY

MANCHESTER City imeonyesha nia kubwa ya kumrejesha beki wa kulia wa Tottenham Hotspur na Hispania, Pedro Porro, mwenye umri wa miaka 24 na kiungo wa kati wa Aston Villa na Brazil, Douglas Luiz (25), katika klabu hiyo kwa mikataba ambayo inaweza kuwagharimu pauni milioni 200. **(Football Insider)**

### DANJUMA ANUKIA UFARANSA

KLABU ya Lyon ya Ufaransa inajaribu kumsajili winga wa Uholanzi, Arnaut Danjuma, mwenye umri wa miaka 26, ambaye alijiunga na Everton kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Villarreal msimu uliopita wa joto. **(Liverpool Echo)**

### BENZEMA SAFARI IMEIVA

MSHAMBULIAJI WA Ufaransa, Karim Benzema, yuko tayari kuihama klabu ya Saudi Pro League ya Al-Ittihad, lakini mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 unaweza kuwa kikwazo kwa uwezekano wowote wa kuhamia Arsenal au Chelsea. **(Standard)**

### ROGERS ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa imeanzisha ombi la kumnunua winga wa Middlesbrough, Morgan Rogers, mwenye umri wa miaka 21, huku kocha Unai Emery akimtaka mchezaji huyo ambaye ameiwakilisha England katika ngazi ya vijana. (Independent)

### MADDISON KUREJEA DIMBANI

NYOTA wa Tottenham Hotspur, James Maddison, mwenye umri wa miaka 27, analenga kurejea kutoka kwenye jeraha la goti kwa timu yake katika mchezo wa raundi ya nne ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City utakaochezwa Januari 26, mwaka huu. **(Telegraph)**

### RODON ATAKIWA LEEDS

KLABU ya Leeds United inafanyia kazi mkataba wa kudumu kumsajili mlinzi aliyeko kwa mkopo Tottenham Hotspur, Joe Rodon, mwenye umri wa miaka 26, ambaye thamani yake ni zaidi ya pauni milioni 15. **(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# OSIMHEN: ILIKUWA LAZIMA TUWAFUNGE IVORY COAST

●●● Akiri wenyeji waliingia na nguvu kubwa huku akiweka...

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Victor Osimhen, amesema ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya wenyeji Ivory Coast katika michuano inayoendelea ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ulikuwa ni mzuri na wa lazima kwa Super Eagles hao.

Osimhen ambaye alitajwa mchezaji bora wa mechi hiyo alishiriki furaha yake wakati wa mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi, akisisitiza umuhimu wa ushindi wa mchezo huo.

Baada ya matokeo ya sare ya 1-1 katika mechi yao ya ufunguzi dhidi ya Equatorial Guinea, Nigeria ilionyesha uthabiti na dhamira, na kupata ushindi muhimu dhidi ya Ivory Coast

Wakati muhimu ulifika dakika ya 55 wakati Osimhen alipofanyiwa madhambi na kuzawadiwa penalti, iliyopigwa kwa ustadi na William Troost-Ekong na kupata bao hilo pekee katika mchezo huo.

Katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi, mshambuliaji mahiri wa Napoli, Osimhen alionyesha wazi furaha yake, akisema, „Ni ushindi mzuri; tulijua tungekutana na timu yenye nguvu ya Ivory Coast."

Akikubali ukubwa wa changamoto iliyoletwa na Ivory Coast, Osimhen aliongeza, „Mechi hii ilikuwa mtihani mkubwa kwetu, na tunafuraha kushinda."

Akiwa na uhakika wa mbinu thabiti katika mechi zijazo, Osimhen alisisitiza mtazamo sawa na walioonyesha dhidi ya Ivory Coast maarufu kama Tembo.

„Katika mechi ya kwanza, tulipata nafasi nyingi ambazo hatukuzitumia. Leo (juzi) haikuwa tofauti; tulidumisha fikra zile zile, na tunatumaini ushindi huu utaleta furaha kwa kila mtu. Tutabeba mawazo haya katika kipindi kilichobakia," aliahidi.

Nigeria sasa inaelekeza mawazo yao kwenye mechi ijayo dhidi ya Guinea-Bissau itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Félix Houphouët Boigny mjini hapa.

Osimhen alisisitiza kutomdharau mpinzani wao, akisema, „Tunalenga kufanya vyema dhidi ya Guinea-Bissau. Bila shaka watakaribia mchezo huo kwa ari, na hatutadharau timu yoyote, kwa kuzingatia kile walichokifanya ili kufuzu."



# KUDUS ALIA UZEMBE GHANA

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KIUNGO mshambuliaji wa Ghana, Mohammed Kudus, anahisi Ghana ilistahili zaidi baada ya kuongoza mara mbili katika sare ya 2-2 dhidi ya Misri katika mchezo wao wa pili wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), uliochezwa mjini Abidjan juzi usiku.

Kudus aliwaweka Ghana mbele mara mbili, lakini Misri walisawazisha na mchezo huo kumalizika kwa kugawana pointi.

"Nimefurahi kurejea. Nilijitahidi sana kurejea kileleni na kuisaidia timu yangu, taifa langu. Ni muhimu kwangu kuwa hapa," alisema mshambuliaji huyo baada ya mchezo huo.

Licha ya mabao mawili kutoka kwa Kudus, Ghana ilinyakua pointi moja pekee kutokana na sare hiyi na nyota huyo wa West Ham hakuficha kufadhaika kwake.

"Ni hisia mchanganyiko. Kama mshambuliaji, unataka mabao yako yawe na mchango kwenye matokeo.

"Tulifanya makosa ya kizembe. Sasa itabidi turudi kazini, tushinde mechi inayofuata kisha tuone kitakachotokea," alisema Kudus.

"Hatujatoka. Lengo linabaki pale pale, ambalo ni kulibeba kombe."

# Ghana bado hawajakata tamaa



**ABIDJAN, Ivory Coast**

KOCHA Mkuu wa Ghana maarufu kama Black Stars, Chris Hughton, ameelezea kusikitishwa kwake kufuatia sare ya 2-2 na Misri katika mchezo wa raundi ya pili ya makundi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Ghana iliongoza mara mbili na kuiwezesha Misri kuchukua pointi moja kwenye mchezo huo na licha ya matokeo ya kukatisha tamaa, Hughton bado anaimani na kikosi chake.

"Tutaendelea kupambana. Ni kweli kwa sasa kuna kuchanganyikiwa sana kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Timu yetu ilistahili zaidi, lakini mpira wa miguu uko hivyo. Inakatisha tamaa. Katika utendaji kama huo, bila shaka tungeshinda. Makosa mawili yalitugharimu. Hatukuchukua nafasi hii kuchukua pointi tatu," alisema.

Osmane aliyeingia kipindi cha pili alitolewa tena nafasi yake ikachukuliwa na Joseph Paintsil.

Hughton alieleza makosa ya winga huyo yalikuwa yanatia wasiwasi na alilazimika kuchukua uamuzi wa kumtoa.

"Kwanza, ningependa kusema tunampenda Osmane. Hata hivyo, ilibidi nimtoe nje kwa sababu makosa yake yalikuwa yameanza kuathiri utendaji kazi wake," alieleza.

Akili ya Hughton sasa iko kwa Msumbiji, mpinzani mwingine wa Black Stars.

"Hakuna tena timu ndogo barani Afrika. Tunajiandaa kwa mechi ngumu dhidi yao.

"Mahesabu tayari yameshafanyika, tunahitaji ushindi ili kutekeleza ndoto yetu na najua tunaiweza." alisema.

# Wachezaji walionyesha dhamira- Kocha wa Misri

**ABIDJAN, Ivory Coast**

BADO hakuna ushindi wowote kwa Misri katika Kombe la Mataifa ya Afrika, lakini hilo halionekani kumsumbua kocha mkuu wa kikosi hicho, Rui Vitoria.

Kocha huyo alikuwa akizungumza baada ya timu yake kutoka nyuma mara mbili na kupata sare ya 2-2 dhidi ya Ghana siku ya Alhamisi.

"Nina imani kamili na timu yangu, nimeona wanaume jioni hii (juzi) ambao walipigana hadi mwisho na tukapata sare.

"Tulionyesha sifa nzuri jioni hii (juzi) dhidi ya Ghana iliyokuwa bora. Wachezaji walitekeleza maagizo yangu kikamilifu. Kulikuwa na nafasi ya kushinda mechi hiyo," alisema Vitoria.

Hata hivyo, kocha huyo raia wa Ureno hakukwepa swali kuhusu jeraha la nahodha wake, Mohamed Salah, ambaye alitolewa dakika za mwisho za kipindi cha kwanza kutokana na kushukiwa kuwa na jeraha la misuli ya paja.

"Kwa sasa, siwezi kusema juu ya uzito wa jeraha lake. Kwa kweli, tuna wasiwasi na tunatumaini sio mbaya sana.

Tutalazimika kuweka hali sawa ya akili kwa mechi ijayo dhidi ya Cape Verde," alisema kocha huyo.



## HABARI MICHEZO

# SERIKALI YAKABIDHI 106M/- KWA NYOTA KARUME BOYS

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WACHEZAJI wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 15 ya Zanzibar (Karume Boys), wamekabidhiwa Sh. milioni 106.7 ikiwa ni motisha kutokana na kutwaa ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-15), yaliyofanyika Novemba, mwaka jana nchini Uganda.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Zanzibar imekabidhi fedha hizo kutokana na ahadi zilizotolewa na wadau mbalimbali kutokana na mafanikio ya Karume Boys katika michuano hiyo.

Akizungumza jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad Rajab, alisema timu hiyo ilikuwa na wachezaji 35 na kila moja atapewa sh. milioni 2.9.

Alisema amefarajika kuona wachezaji hao vijana wamejitokeza na wazazi wao na kushuhudia fedha hizo zilizotolewa na wadau zimekwenda kwa walengwa kama ilivyokusudiwa na itaongeza chachu ya kufanya vyema katika mashindano mengine.

Waziri huyo aliwashukuru viongozi waliojitolea katika hafla hiyo na kusema uamuzi huo utaendelea kuwapa nguvu vijana na kuimarisha sekta ya michezo. Mmoja wa wazee waliohudhuria hafla hiyo, Masoud Shaaban Kombo, amewapongeza viongozi na wadau kwa kuichangia timu hiyo na kuwataka kuendelea kuwachangia vijana ili kuzidisha hamasa.

„Tunaendelea kuwashukuru wadau wote waliojitokeza kuchangia na kutoa zawadi kwa wachezaji wetu wa timu hii ya taifa, michango yao imesaidia kutoa hamasa kwa wachezaji na hata wadau wa soka kwa ujumla hamasa ambao kila kijana angependa kujituma na kufanya vizuri katika soka," alisema Masoud.

Aliongeza mchakato wa kugawa fedha hizo umefanyika vizuri na kuwaomba kudumisha ushirikiano ili vijana wapate zaidi fursa ya kucheza soka na kujipusha na vitendo viovu.

Adam Masoud Shaban, akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema wamepata faraja kutokana na hatua iliyochukuliwa na amewaomba wadau kuendelea kuinga mkono timu hiyo, ili ifanikiwe katika mashindano mengine ambayo Zanzibar itashiriki.

## Taifa Stars yatakiwa kuiheshimu Zambia

INATOKA UK. 24

dimbani ikiwa na mipango ya kujilinda na kwa kufanya hivyo, itapoteza mchezo huo na kuondoa matumaini ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

„Nafikiri kwanza tunatakiwa kucheza kama timu zilizofuzu AFCON, kwa maana tulivyocheza mechi iliyopita dhidi ya Morocco ni kama vile ndio tunawania kufuzu wakati kumbe tayari tuko katika fainali. Sasa unapocheza AFCON unahitaji matokeo na ulinzi, hivyo mechi ijayo tucheze kwa nidhamu ya ulinzi lakini washambuliaji pia wawe makini.

Tuwaghasi wapinzani kuliko kuwaacha wacheze. Tukiwaghasi sana kwa lengo la kuwanyanganya mipira watafanya makosa na tutawahukumu kupitia makosa yao," Badru alisema.

Kocha huyo aliongeza uamuzi wa kucheza kwa mfumo wa kuzuia ulipaswa kufanywa katika mechi za kufuzu lakini kwa sasa lazima timu ionyeshe wao ni bora na ndio maana wapo kwenye michuano hiyo.

„Lazima tujue sisi tayari tumeshakuwa bora Afrika ndio maana ni tupo AFCON na kuzidi nchi nyingine, lazima tuonyeshe ubora wetu lakini tusiache kumheshimu mpinzani.

Tusiingie uwanjani kwa hofu kama ilivyokuwa katika mechi ya mwanzo na kukaa sana nyuma, ulitugharimu, huwezi kukaa nyuma na kuzuia kwa timu nyenye ‚maprofeshno' wengi wazuri, lazima watakuadhibu tu.

Mechi dhidi ya Morocco tulikukubali sisi ni wadogo na kuwaachia wakubwa wacheze, sasa ukimwacha mkubwa acheze lazima atakuadhibu lakini ukimpiga presha lazima atafanya makosa na itakupa wewe nafasi ya kumwadhibu," aliongeza Badru.

Mkenya Francis Baraza, Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, alisema bado Stars ina nafasi ya kushinda mechi dhidi ya Zambia na kikubwa waondoe hofu lakini wacheze kwa nidhamu.

Baraza alisema ‚plani' ya mwalimu (Adel Amrouche) katika mechi iliyopita ilikuwa nzuri ila tatizo mabeki na viungo hawakuisogezi timu mbele hivyo kuacha nafasi kubwa kati yao na washambuliaji.

„Walikuwa wanacheza nyuma sana katika eneo lao na kuwapa nafasi wapinzani kuwashambulia, hivyo wanatakiwa kubadilika katika mechi dhidi ya Zambia. Waondoe woga lakini wanatakiwa kuwa waangalifu kwa sababu Zambia nao wana pointi moja, mechi lazima iwe ngumu.

Lakini Kocha wa Stars nafikiri anapaswa kumwanzisha Samata (Mbwana), Msuva (Simon) na Feitoto (Feisal Salum), kwa pamoja ili kuleta presha kwa wapinzani, naamini hiyo mechi wakiweka presha kubwa katika kushambulia watashinda," alisema Baraza.

Morocco yenye pointi tatu ndio vinara wa Kundi F wakifuatiwa na DRC na Zambia zenye pointi moja kila mmoja huku Stars ikiburuza mkia.

## Kramo 'OUT' Simba, Yanga moto ule ule

INATOKA UK. 24

kuhusu wachezaji wa kigeni tayari wameshaanza kuwasili, hadi siku hiyo wote watakuwa wamefika na wako tayari kuanza kazi," alisema Ahmed.

Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize, alisema amekumbuka shangwe za mashabiki wao kufuatia kupata ushindi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

„Wananchi, wanachama na mashabiki wa Yanga, wana hamu ya kutuona tukicheza na kupambana uwanjani, ‚wametumiss na tumewamiss' sana, tulikuwa nao pamoja, tuliwapa furaha na kushangilia kwa pamoja, naamini tutakuja kivingine tena, yale yamepita, tutakuja mara mbili zaidi ya mwanzo," aliahidi Mzize.

Naye Maxi Nzengeli alisema ni furaha kuona mashabiki wanasafiri kuifuata timu na wao kama wachezaji watapambana kuhakikisha wanapata ushindi ili kuwapa amani.

„Tumewamisi' mashabiki wetu, wao hutufuata popote tuendapo, wanatushangilia kwa nguvu zote na kutupa morali, furaha na kujituma kuipambania nembo ya klabu, leo hii hatuwaoni kwa sababu mechi zimesimama, na sisi tulipata mapumziko kidogo, nina imani tutakutana tena na tutakuwa na wakati mzuri kwa mara nyingine," alisema kiungo mshambuliaji, Nzengeli.



Meneja wa Wateja Maalum wa Kampuni ya Tigo, Mary Rutta (Kushoto) akizungumza na waandishi wa habari jana wakati akitangaza washindi wa droo ya nane ya promosheni ya magifti dabodabo, kulia ni mmoja wa washindi hao, Farida Kyeumbile. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Promosheni Magift Dabo bado wiki 3

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI promosheni ya magifti dabodabo ikiwa imebakisha wiki tatu kukamlizika, kampuni ya tigo imewataka wateja wake kuendelea kushiriki ili kupata nafasi ya kushinda zawadi mbalimbali ikiwamo zawadi kubwa ya magari mapya na fedha Sh. milioni 30.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana, wakati wa kutangaza washindi wa wiki ya nane wa promosheni hiyo, Menaja wa Wateja Maalum wa Tigo, Mary Rutta, alisema kwa sasa wanaelekea ukingoni hivyo anawataka wateja kuchangamkia fursa ya kushinda zawadi mbalimbali.

„Bado zawadi zipo na zitaendelea kutolewa kama tulivyotangaza, kuna zawadi kubwa za magari mapya mawili na fedha Sh. milioni 30, hizi zitatolewa kwenye droo ya mwisho, wateja wetu waendelee kucheza," alisema Mary.

Aliongeza kwa wiki hii ya nne, washindi mbalimbali wamepatikana na tayari wameanza kuwakabidhi zawadi zao. „Leo (jana), hapa tunawawakilishi wa washindi wetu wa wiki ya nane, tuna washindi wa sh. milioni moja, Sh. milioni tano na vifaa vya umeme vya majumbani, wote hawa watakabidhiwa zawadi zao," Mary alisema.

Mmoja wa washindi, Mohamed Salum kutoka Mwananyamala jijini ameishukuru kampuni hiyo kwa kuendesha promosheni inayowafaidisha wateja wao.

„Nilipigiwa simu Jumanne kupewa taarifa hii ya ushindi, kwa kweli nashukuru sana na leo (jana), nimekabidhiwa zawadi yangu ya sh. milioni moja," alisema Salum.

Aliongeza fedha hizo alizopata zitamisaidia katika kuendeleza shughuli zake na kuweka wazi wakati anapewa taarifa za ushindi alikuwa anampeleka mtoto wake shule na jana ndipo akabidhitisha kupata zawadi hiyo.

Michezo

Jumamosi Januari 20, 2024

Nipashe

Osimhen: Ilikuwa lazima tuwafunge Ivory Coast UKURASA 21





Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akikagua Uwanja wa Laurent Pokou ulioko San Pedro, Ivory Coast ili kujifunza maandalizi yaliyofanywa na wenyeji wa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), yanayoendelea nchini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAIFA STARS YATAKIWA KUWAHESHIMU ZAMBIA

## ●●●Pia yakumbushwa kucheza kwa nidhamu na kuondoa hofu ili...

**Na Oliver Albert**

KATIKA kuhakikisha wanapata matokeo chanya, nyota wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wametakiwa kucheza ‚kikubwa' na kutokuwa na hofu ya aina yoyote kuelekea mechi yao ya pili ya Fainali ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), dhidi ya Zambia itakayofanyika kesho.

Stars iliyoko Kundi F, ilianza fainali hizo kwa kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Morocco na itamaliza hatua ya makundi kwa kuwakabili Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Januari 24, mwaka huu.

Taifa Stars pia wametakiwa kumheshimu na kujilinda kwa nidhamu dhidi ya mpinzani wao Zambia maarufu Chipolopolo na vile vile kutumia vyema nafasi watakazotengeneza ili kupata ushindi katika mchezo huo na ujao dhidi ya DRC.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha na mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Boniface Mkwasa ‚Master', alisema Stars inatakiwa kubadilika kiuchezaji katika mchezo huo kwa sababu wanafanana viwango dhidi ya Zambia.

„Mechi iliyopita dhidi ya Morocco ilikuwa ngumu kwa sababu lazima tukubali tulikutana timu yenye ubora wa viwango tofauti kabisa.

Wachezaji wa Stars hawakuwa wakifanya mashambulizi bali walizuia sana na kufanya wawe na idadi kubwa nyuma kwenye goli lao, sasa wakati mwingine inapelekea kufanya makosa mengi na hata kumzuia kipa asione mpira kwa urahisi,“ alisema Mkwasa na kuongeza;

„Mechi ijayo wanatakiwa kubadilika kiuchezaji kwa sababu Zambia tunafanana nao viwango, lakini wawe makini katika kuzuia, kukaba na kutotumia nguvu kubwa kipindi kimoja, bali wawe bora kila kipindi. Pia waache kukaa nyuma sana kulinda goli, bali waongeze idadi kubwa ya watu mbele ili wafanye mashambulizi sana timu ipate mabao, na wasisahau kuongeza utulivu katika upigaji wa pasi, „ alisema Mkwasa.

Naye Kocha mzoefu, Kennedy Mwaisabula ‚Mzazi' alisema ni lazima wachezaji wa Stars wamheshimu mpinzani wao kama wanahitaji kuvuna pointi katika mchezo huo wa kesho.

„Ukiangalia mechi dhidi ya Morocco, Stars walianza kwa kasi ya kushambulia na wapinzani wakawa kama wanatuchora tu, lakini baadaye mambo yakabadilika kwa sababu walishatusoma. Sasa hiyo ni kwa sababu hawakumheshimu Morocco, inatakiwa kumsoma kwanza mpinzani wako yuko vipi, ndio maana wale karibu timu nzima ni ‚maprofesheno', wanacheza Ulaya.

Hivyo wanajua nini wanafanya na walitumia makosa yetu kutuadhibu. Mechi ijayo na Zambia, Stars wanatakiwa kuwa makini hasa katika ulinzi, wapinzani sio wakali sana kama ilivyo DRC, wakicheza kwa nidhamu, bila hofu tunawamudu kabisa na tunaweza kuwafunga,“ alisema Mwaisabula.

Mohammed Badru, Kocha wa timu za vijana Azam, aliliambia gazeti hili Stars wanatakiwa kucheza ‚kikubwa' katika michuano hiyo ya AFCON na uwezo wa kushinda wanao.

Badru alisema kamwe Stars isishuke

INAENDELEA UK. 23

# Kramo ‚OUT' Simba, Yanga moto ule ule

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI jina la kiungo wa Simba, Aubin Kramo, likiondolewa katika orodha ya wachezaji ambao wataitumikia timu hiyo katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, nyota wa Yanga wamesema ‚wamemiss' shangwe kutoka kwa mashabiki wao.

Taarifa zilizopatikana kutoka ndani ya Simba zinasema uamuzi huo umetokana na kiungo huyo kutakiwa kufanyiwa matibabu zaidi na atafanya program maalumu ya mazoezi chini ya uangalizi wa madaktari huku akitarajiwa kurejea uwanjani kuanzia Mei, mwaka huu.

Chanzo hicho kilisema kufuatia hali hiyo, mabosi wa Simba wameamua nafasi ya kiungo huyo itachukuliwa na Freddy Michael ambaye ni mmoja wa wachezaji wapya waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema wamefanya maboresho ya kikosi kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi lakini suala la Kramo bado yupo katika uangalizi wa madaktari ili awe fiti kwa asilimia 100.

Kajua alisema endapo kutakuwa na taarifa rasmi kuhusiana na nyota huyo itawekwa wazi lakini kwa sasa anaendelea kujifua ili kujiimarisha.

"Tumefanya usajili kulingana na mahitaji ya kocha wetu, tumesajili wachezaji ambao wametakiwa ili kuimarisha kikosi cha timu yetu, hakuna mchezaji wa kigeni aliyezidi," alisema Kajula.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya kutoka visiwani Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi wachezaji walipewa mapumziko ya siku 10 na watarejea mazoezini ifikapo Januari 25, mwaka huu.

"Mashine zote mpya zitakuwepo na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >